# Malezi

## ya kuhani mtarajiwa.

Malezi ya kuhani mtarajiwa.



MaarifaMtandaoni.com, RohoYaUnabii.Org

KUKUZA MTOTO WA KIUME KATIKA TABIA BORA, AJIKIMU, AWE KUHANI NAKUSIMAMIA NYUMBA YAKE (Kukuza mwana awe mlei- wameandikiwa watoto wa kiume na wazazi)

Wengi wameandika vitabu vya kukuza watoto wa kiume kwa waumini. Kukuza mtoto wa kike hakuna tofauti kubwa na kukuza mtoto wa kiume isipokuwa pale majukumu ya jinsia yanapotofautiana, kama vile ambavyo Mungu alituagiza. Mungu ndiye mzazi mkubwa, Maandiko ndiyo kitabu cha malezi kikubwa, vingine ni kujazia hicho. Jambo kubwa la kuwasaidia watoto wetu, ni kuwafanya waweze kuishi bila sisi. Waweze kukabiliana maisha kwa mahusiano na Mungu, jumuiya yaani shuleni au kazini, ushirika, na familia zao.

1. *Mbingu na dunia ndiyo vitabu vya mtoto wa kiume, kabla hajaanza kujua kusoma au kuandika, kama Zaburi 19 inavyosema. Zaburi 144: 12-15 yasema, 'Wana wetu na wawe kama miche waliokua ujanani. Binti zetu kama nguzo za pembeni zilizonakishiwa kwa kupamba hekalu. Ghala zetu na zijae akiba za jinsi zote. Kondoo zetu na wazae elfu na makumi elfu, mashambani mwetu ngombe zetu na wachukue mizigo, kusiwe kushambuliwa. Wala kusiwe kuhamishwa. Wala malalamiko katika njia zetu. Heri watu wenye hali hiyo. Heri watu wenye Bwana kuwa Mungu wao."*

Tafsiri ya Mungu ya mwanamume ni zaidi ya kuonekana kwa nje; maana Ezekieli 22:30 yatuambia, ni mtu atakayekuwa tayari kutengeneza pale palipobomoka. Kuwa mwanamume katika Neno la Mungu ina maana kiroho, kiakili, kihisia na kimwili. Mtoto anasaidiwa nyumbani, kwenye jumuiya, shuleni na kanisani

Baada ya kupata watoto lazima tuwe na mipango maana Mungu ametupa wana kama mawakili, ni bustani yetu kupalilia, mpaka wakue na kukomaa. Hatuwezi kukaa tu na kufikiri mambo yatajipa yenyewe. Chakula na nguo havitoshi kukamilisha malezi ya watoto.

Watoto wetu wa kiume watakuwa viongozi katika jumuiya zao, watakuwa makuhani kwenye nyumba zao na watakuwa kaka zetu kule mbinguni siku moja. Tunamtayarisha mtoto wetu wa kiume kuwa mume, baba na muumini katika nyumba ya Mungu. Hii ni safari inayohitaji muda mwingi, na imekita kwenye mhimili wa Neno la Mungu.

Neno la Mungu ndiyo mwanzo na mwisho katika malezi (alfa na omega). Neno la Mungu ndiyo usalama wetu pekee wazazi na watoto wetu. Hebu uweze kuvuna matunda ya kazi yako, ya uaminifu kwa Mungu; na uweze kuwasaidia watoto wako kuwa mashujaa, wanaochukua majukumu na kuzaa matunda mengi ya haki. Luka 2:52 yasema, Yesu alikua kwa kimo na hekima akimpendeza Mungu

na wanadamu. Miaka ya kumi na, (teenage), si lazima iwe na shida za ujana na uasi, bali ya uzalishaji (productivity) kwa mwana, wazazi na jumuia. Tusichoke kutenda mema. Maana siku moja 'baba yako na mama yako watafurahi , na yeye aliyekuzaa atashangilia'. 'Sisi kama wazazi tuwachukue watoto wetu kwenye semina za injili au walei, tusiwaache. Tuwachuku katika shughuli tunazomfanyia BWANA ili wajifunze kwa matendo na kuipenda kazi yake BWANA.

Kukuza mtoto wa kiume ampendaye Mungu yahitaji kuwajibika (commitment), maana watoto wetu wa kiume siku hizi wana changamoto ya kujishughulisha kwa bidii, kwenye taaluma na hata kazi za mikono. Asilimia 90% ya mashamba Afrika hulimwa na wakina mama watu wazima. Pia Asilimia 80 ya waumini wengi kwenye nyumba za ibada ni wana wa kike, na ndiyo waonekana na hari ya kwenda shule na kusoma vitabu kwenye nchi nyingi. Zamani kuna masomo ya hisabati au fizikia yaliaminika kuwa masomo ya kiume; na ndio walichukua namba za juu. Utafiti wa Dr Nedley Marekani unasema kwamba namba hizi zataka kufanana na za watoto wa kike siku hizi. Akaongeza kwamba watoto wa kiume wanaona hakuna haja ya kujishughulisha siku hizi kwani kupata mke wa kuoa ni rahisi, wala uhitaji mahari kama zamani.

Wasichana siku hizi ndio wanafuata wavulana. Hii inawafanya wasiwajibike au wasione changamoto au ari ya kufuatilia kitu. Anasema pia watoto wengi wa kiume wanaweza kumudu maisha yao wakitegemea wazazi au mke mpaka uzeeni, endapo mke atashtuka na kumwacha, mke huyu atachukua watoto aende nao, na mume atarudi kwa wazazi na kuwategemea.

Mtoto wa kiume ameumbwa kwa mfano wa Mungu naye aliumbwa kabla ya mwanamke. Kusudi lake halikuwa kuongeza na kujaza nchi kwanza, bali kumiliki na kutiisha nchi. Wana wetu ni lazima wajue hili kwanza. Mtoto wa kiume alipewa kazi ya bustani hata kabla ya maanguko ya binadamu. Utii kwa Mungu na mzazi, ndiyo somo la kwanza kwa wana wetu. kisha mipangilio,Ustadi, taaluma, kutawala nafsi, na kazi za mikono. Hivi vinamsaidia kukana nafsi na kutawala nafsi na kuitafutia riziki familia. Zamani mtoto wa kiume Afrika ndiye aliyetunza wazazi, na kutegemewa na dada zake au wadogo zake kama ndiye mtafutaji, mshauri na kiongozi. Jambo hili limeanza kupungua kwa kiasi fulani.

Japo hiyo ni takwimu ya Marekani, ila unapoona mwenzako ananyolewa, wewe anza kutia maji kichwani. Nchi hii ya Marekani inaweka viwango mara nyingi, japo ni vibaya kama vile vya ushoga, na watu wengine wanafuatilia kirahisi. Mengi siku hizi watoto wanayoona kwenye vyombo vya habari, hasa runinga, yanaigizwa na vyombo hivi vyawa kama mzazi. Hii ni hatari maana vyombo vingi vya habari, vina machache mazuri, hata kwenye matangazo, watu wanavyozungumza na kuvaa kunakuwa na walakini.

Nilipokuwa mtoto, ilikuwa matusi kumwita mvulana 'msichana;' ila siku hizi hata wavulana wenye nguvu na akili wameingia desturi za maovu kama ushoga, jambo ambalo lilikuwa mwiko, hata kwa wale wasiomcha Mungu. Watu wa nchi

kama Ufilipino wanasemekana wanaongoza katika takwimu ya kufanya upasuaji wa wanaume kujibadilisha kuwa wanawake ili maisha yao 'yawe rahisi'. Hii ni kutojua kwamba katika uumbaji, mwanamume ndiye alitangulia naye ni kichwa, na anapaswa kuheshimiwa na mwanamke. Na hata hivyo mwanamke ni mfanya dhambi wa kwanza na sidhani kama hilo linavutia mtu ye yote.

Herodi aliua watoto wa kiume. Farao pia, alijua akimaliza watoto wa kiume, taifa limekwisha. Hata Balaam aliangusha wanaume 24,000 wa Israeli, akijua akimaliza hao amemaliza taifa. Mungu amempa mtoto wa kiume na wanaume karama na jukumu ambalo wana wa kike hawakupewa, hivyo tunapokuza watoto wa kiume tuangalie hili. Wakina baba wakae na watoto wa kiume na kuwafundisha kwa matendo. Wanasema wakina baba wengi hukaa pungufu ya dakika nne kwa siku kuzungumza na watoto wao.

Yapasa kuwa na uchaguzi wa mambo mengi kama vile marafiki, miziki tunayosikiliza, vitabu tunavyosoma, elimu tunayopata, kanisa tunalohudhuria, nguo tunazovaa, na mengine mengi. Wazazi tusome neno la Mungu ili tupate majibu, na viwango vinavyofaa, pia tujifunze kuwa waumini waliokomaa, na kuhudumu pamoja. Hata wale wazazi solemba wanaweza kukuza watoto wanaompenda Mungu. Tunaona Timotheo, na bibi yake Loisi na mama yake Yunia, wakimsaidia Timotheo kuwa shujaa aliyehudumu wengi kama mlei na kisha mchungaji.

Lazima uwe na malengo na mipango ya mwaka mmoja. Huwezi ukafanya yote kwa pamoja, weka ramani kidogo, kile unachotaka ukipate, watoto wahitimu toka nyumbani. Watoto wakiwa wadogo wanakuwa kama sponge; inayonyonya maji mengi. Wanashika mengi ya sayansi na kukariri sana. Tumia muda huu kuwafundisha kutoka kitabu cha viasili na dunia. Mafundisho ya 1 Wakorintho 13 ya upendo, ni muhimu kwa watoto na sisi.

Daima watoto wetu wafundishwe uumbaji wa Mungu na si uibukaji, (evolution). Hili tulipatie kipaumblele; 1 Kor 3:19. Tutumie msaada wa mababu na mabibi kuwasaidia watoto.

Watoto wafundishwe kujenga nyumba, kushona, kupika, kulima na ustadi mwingine. Wafundishe watoto kuzungumza hadharani, kupanga muda wao, na kutathmini wanavyoendelea. Furahi nao kwa walichokiwezea. Wafundishe mashujaa wa mifano ya Neno la Mungu kama Daudi, Nuhu au Ibrahimu. Mwulize kijana wako mashujaa wake ni wapi? Ni watu wa filamu au michezo ya compyuta? Je, awezaje kuwa mshumaa au mwanga wa nyumba yake?

Soma vitabu kama '10 Boys Who Changed the World,' kilichoandikwa na Irene Howard. Je, anawahusudu (admire) watu ambao hawampendi Mungu kama Samsoni? Je, anasoma vitabu vya namna gani?

Maisha ya mwanamume yamejaa maamuzi mbali mbali, na kutenda kutokana na maamuzi, tuwatayarishe vijana wetu kuchukua majukumu kwa kuamua mambo inavyotakiwa. Watayarishe vyema kisha waachiwe nafasi wafanye maamuzi, na wanapokosea wajue kusahihisha. Jifunzeni hata toka kwa wadudu

kama siafu, na mifano ya watu kama ya kijana Yusufu, Yethro, Abigaili, Msamaria mwema, Boazi na wengineo.

Usipokuwapo anafanya vitu vyema? Je, anasalimu watu?, anafanya kazi za nyumbani? Angalia kama anatumia muda wake vizuri, na kuacha vitu vyake katika mpangilio na usafi. Je, anajua kutatua matatizo, au anasahau majukumu yake? Je, anajua muda ni mali na hasemi nitafanya kesho?

Mpeleke polisi, au kotini kutokana na umri na kisha mjadili kesi za kawaida. Soma visa kama vya Akani na Samsoni mjadili. Je, apenda kutoa udhuru au kutia chumvi, na kuweka ahadi asizotimiza? Je, anachukua vitu vya watu bila ruhusa? Je, anapenda umbeya na kushuhudia watu uongo? Tusiwakinge sana watoto wetu na maumivu au kushindwa. Mara nyingine ni lazima washindwe ili wajifunze, ila wasiwe na woga wa kujaribu tena. Soma habari za mashujaa 30 wa Daudi (1 Mambo ya Nyakati 11). Pia soma kuhusu mashujaa wa matengenezo kama Luther, Zwingli, Tyndale, Knox, na Huss. Je, aweza kukubali kukosolewa na ajifunze? Je, ana ujasiri wa kujua amefanya dhambi akatubu na kuiacha? Je, anaweza kusema amekosa na kuungama? Je, anaogopa watu zaidi ya Mungu?

Mwanamume ni kichwa cha familia, kama vile Kristo alivyo kichwa cha kanisa, angalia tabia za wanaume kama Nuhu, Ayubu, Ibrahimu, Musa, Daudi. Ibrahimu shujaa alisifiwa, 'Kwa maana nimemjua ya kwamba atawaamuru wanawe na nyumba yake baada yake waishike njia ya BWANA wafanye haki na hukumu.' Mtoto wa kiume yapaswa ajue mafundisho makuu ya imani kwa uhakika na kutofautisha mafundisho ya uongo-doctrines. Maana atakuwa kuhani wa mji wake, na hata nyumba ya ibada. Awahoji wachungaji na viongozi wa kiroho vile wanavyoamini. Je, injili ni nini? Inawaathirije maisha yao? Kumbukumbu 6:7,8 wafundishwe watoto na wakariri. Wazazi wasaidie watoto wa kiume kuwa walimu.

Kujifunza uongozi ni muhimu. 1 wafalme 3:9; 'Nipe mimi mtumwa wako moyo wa adili niwahukumu watu wako, na kuwapambanua mema na mabaya, maana ni nani awezaye kuwahukumu hawa watu wako walio wengi?' Hapa Sulemani aliomba hekima na uongozi. Twatoa mifano kwa wana wetu kuwa mahakimu wa haki. Tunapowaadabisha, tunainua sheria ya Mungu, na kuwasaidia katika mausia ya Bwana. Twafundisha kuzungumza na marafiki zao wanapowakosea, ili kuweza kurudisha uhusiano mwema, kusudi waweze kuwasaidia watoto wao wanapofanya makosa ya sheria ya Mungu. Hakikisha adhabu zako kwa mtoto zinalingana na upendo wako, endapo adhabu zako zinazidi upendo kuna walakini. Twasema vile tukijua wote ni binadamu tunakosea, na kila mtu ana mizoga fulani katika shuguli ya kulea, ila adhabu iwe ya upendo, kumrudi mtoto, na si hasira. Usimpe mtoto adhabu ukiwa na hasira, ngoja ipoe, kisha uzungumze naye, na kisha umpe adhabu.

Je, mtoto aweza kuwaongoza wengine kwa unyenyekevu na kugawa kazi, hata kuzisahahisha na kutathmini? Angalia "Brother Offender Checklist" na "21

Rules of This House" kwenye website ya maneno hayo. Muwe na koti nyumbani, ili muamue lipi lahitaji adhabu na lipi lahitaji maonyo. Angalia kwenye maandiko adhabu za manabii, za watu na za mitume. Orodhesha dhambi ambayo mtoto anapambana nayo, panga adhabu, na matokeo ya kukataa maonyo. Je! mamlaka yana majukumu gani, tunapaswa tutendeeje mamlaka. Je! mwana wako anakubali kufundisha wengine, kama darasa la watoto au vijana wenzake kanisani?

Mtoto wa kiume afundishwe kutokuwa na tamaa ya vitu vya mtu, na kushukuru kwa alivyo navyo, maana tamaa. Utauwa na kuridhika ni baraka kubwa, kwani tulikuja duniani bila kitu na tutaondoka bila kitu. Pale anapokosea afundishwe kuomba msamaha. Kwa vile atakuwa kiongozi afundishwe kutumia mamlaka na majukumu kwa hekima. Mfano wa waliotumia madaraka vibaya ni mafarisayo, na waliotumia madaraka vizuri ni Nuhu, Ayubu Eliya, n.k. Ajue kwamba madaraka ni kuwa mhudumu au mtumishi wa watu na wala si dikteta wa kunyanyasa watu. Ajue kufanya kazi kwa mikono yake ili aweze kukidhi mahitaji yake na ya wengine. Apaswa kuanza kufunga na kuomba akifika miaka kumi na miwili hivi, maana mengi hayawezekani pasipo maombi na kufunga. Ajue kwamba mke na watoto wake watahitaji nguo, chakula na makazi na hivi ni sababu tosha ya yeye kujifunza kusali na kufunga.

Ukengeufu au upotofu waanza pole pole, kama vile kipima joto kinavyoongezeka; hivyo agundue kwamba baada ya muda atajikuta mbali. Ajifunze kutoka kwa wanaume wenye hekima na wenye tabia njema, maana wanaume hawa wamepitia maisha ya ushindi na maanguko, ili asikanyage pabaya, na kudidimia. Majaribu yanaonekana mazuri, ila hayasemi ukweli wote, asijaribu kupambana na majaribu bali amwuulize Mungu kutii na kuepuka mialiko ya kufanya uovu, kwani pambano ni la Mungu unapochagua, kutii sheria yake.

Kwa nini ni vizuri kijana asijihusishe na nyimbo nyingi kama za Rock muziki na za dansi? Kwa sababu zina uovu, watu wengi wanaoimba wanapendelea uasi wa sheria za Mungu, na kujiingiza kwenye dini za kuabudu miungu mingine zaidi ya Mungu wa Ibrahimu, wanajishughulisha na vileo au madawa ya kulewa, wanafundisha mambo ya giza bila kujua na pia wanafanya mambo ya kiroho yapungue, wakiongeza wasiwasi na kutotulia kwa moyo.

Elimu ni nzuri ila, anza kusoma vitabu mapema, kabla mambo hayajaribika. Mweleze kijana pia. Yaani asisome kitabu cha kuwa na ndoa nzuri baada ya kuachana na mke, ila kabla. Kuelimika na kusoma ni vitu viwili tofauti, unaweza kusomea shahada kubwa ila usielimike. Na pia kupata pesa na kufanya kazi ni vitu tofauti. Neno la Mungu limehakikishwa kwa kila hali ili lisaidie kwa mafundisho, kuonya makosa, kuongoza, kuadabisha kwa haki, ili mtu awe kamili na apate kutenda kila tendo jema.

Mtoto ajifunze kutii utawala, maana hata yeye siku moja aweza kuwa kwenye shuguli ya uongozi. Huwezi kuongoza watu kama wewe hujui kuwa mfuasi.

Tunaambiwa katika Maandiko matakatifu kwamba tuwaheshimu na kuwatii wanaotuongoza, ili kazi yao isiwe ngumu au ya huzuni, maana watatoa hesabu kwa yale wanayofanya. Angalia tu shuguli ambazo serikali ya kawaida inasaidia raia. Tunaelewa kwamba tuna viongozi waovu, ila kwa kawaida viongozi ni msaada mkubwa na hatuwezi kamwe kuishi bila viongozi. Endapo wazazi tunafanya kazi ya viongozi kuwa ngumu au tunawadharau, watoto wataiga.

Kusamehe ni muhimu kwa mtoto wa kiume, na kutosamehe ni kama kunywa sumu na kutegemea mwingine afe. Na pia tukumbuke hata sisi tumewakosea wengine na wanatusamehe. Wapaswa kuwa huru kwa aliyekukosea na si mtumwa wake. Hata hivyo tunasamehewa tunavyosamehe.

Mwana ajifunze kusamehe, na kumwambia Mungu uchungu alio nao, na kumwomba aondoe uchungu huu, asiseme uongo bali kweli ya moyoni kwa Mungu, kwani BWANA anao uwezo wa kutoa uchungu na chuki yote, na atashangaa moyo wake utakuwa mwepesi. Mke, watoto na hata wazazi wanaweza kumkosea. Ila twapasa kujua jinsi ya kutatua haya matatizo, kwani tumeambiwa kwamba ni vyombo dhaifu, hivyo twahitaji hekima ya kuenenda nao. Ajifunze kumwachia Mwenyezi Mungu shida yake hiyo, na ikirudi mawazoni amwachie tena, mpaka itoke kabisa.

Kuweka visasi na chuki ni kitu cha kuangamiza kabisa, Je, tunawezaje kutoa mawazo machafu? Mawazo machafu yanakuja kwa kila binadamu Je, tunayaondoaje? Wengi wanakosa kujikana nafsi na kuzungumza lolote, kuwaza au kutenda chochote. Je, ana hasira anayoshindwa kuikabili? Au mawazo mabaya? Zaburi 119:110 yasema, tuweke neno lake mioyoni mwetu ili tuondoe mawazo machafu, kisha kama Yoshua, tuchague nani tutamtumikia kila siku. Tuchague kumtumikia Mwenyezi naye atatuondolea mawazo machafu. Mawazo yetu lazima 'Tuyaangushe na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mwenyezi Mungu, na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii BWANA;' 2Kor 10:5. na hatimaye, mwishowe tufikirie yote mazuri, ya ripoti njema na ya staha.

Udadisi wa mtoto uweze kukuzwa ili aweze kubuni na kuvumbua mambo. Mpe mtoto vifaa na muda, usiwe unajali sana kwamba ataharibu vitu, au anapoteza muda. Watu waliovumbua duniani walihitaji muda, watu kuwaamini na kutokuwa na presha au misukumo mingi. Ili mtoto aweze kuvumbua anahitaji maarifa katika masomo tofauti. Mungu ndiye mvumbuzi mkubwa, usipoteze muda wako kuvumbua uovu utakaongamiza watu kama wale waliovumbua mabomu ya nuklia!

Kitu kikubwa katika uvumbuzi ni kutokata tamaa. Thomas Edison alifanya majaribio 1,000 yaliyoshindwa ila alivumbua taa na mengineyo. Aligundua njia 1,000 za kutofanya majaribio kwa njia hizo (1,000 ways not to go). Usikate tamaa ushindwapo, jifunze kutokana na makosa na usonge mbele, utapata majibu.

Mtoto wa kiume ameumbwa avumbue nyimbo, program, vitu, mbinu, sanaa, vitabu, zana, na mengineyo. Hebu uwe mvumbuzi kama Mungu

alivyokupangia, kuhudumia dunia, na kuishi maisha yenye maana. Ila usisahau afya ya mwili wako kwa kufanya mazoezi ili usiwe lege lege ukikaa kwenye maabara siku nzima bila kuona jua, na kupata hewa bora!

Mtoto wa kiume, ajifunze kuvumilia, na ajifunze kutunza urafiki. Asiwe mtu wa kukasirika ovyo ovyo na kushindwa kukarabati urafiki. Mara nyingi kama binadamu tunashindwa mengi, ila ujasiri na kujaribu tena na tena ni muhimu. Tunaona hata Mungu hatuachi tunaposhindwa na bado anakarabati maanguko yetu yaliyotokea kwenye bustani ya Edeni, Mwanzo 3.

Je, napaswa niwe wapi (belong)? Mara nyingine unaweza kuona kwamba haufai kuwa mahali fulani. Kwa kweli mbinguni ndiko kwetu sisi wote, huko ndiko tutapoona ni maskani yetu kamili. Usipoteze muda mwingi kuona kama unafit hapa, maana Mwenyezi ameenda kututayarishia makao, na hivyo mara nyingi tutajisikia tu wageni hapa, ila tuweke nia na shabaha yetu kwenye ile nchi ya Paradiso. Afadhali kuishi kama mgeni hapa ukijitayarisha kwenda mbinguni, kuliko ujisikie mwenyeji na mwishowe ulie na kusaga meno. Tutakapolenga mbingu, hata ya dunia itakuwa rahisi kuyakabili, ila tukilenga dunia tu, tutakosa mengi.

Kutenda haki ni muhimu la sivyo mvulana anakuwa mtumwa wa tamaa zake na kutojikana nafsi. Kutendea watu wote haki ni muhimu, na pia kuwiwa na upendo na watu. Twaona mfalme Sulemani alihukumu kwa haki, ila alipoanza kutojikana nafsi, kwa kuchukua wake wengi, alipoteza haki za watu, na kuharibu mahusiano na Mungu. Mara zingine vijana wa kiume wanafikiri haya hayawezi kuwapata wao. Wanasema tukifikiria kwamba haya hayawezi kutupata, basi tu wenye hekima kuzidi Sulemani, wenye nguvu kupita Samsoni, na tunampenda Mungu kuliko Daudi.

Maisha ni kufanya kazi, kusoma, kujenga, kuwekeza, usiwe mvivu na kukaa tu. Usikae kivivu kijiweni (jobless corner) mpaka nguo kuchanika kwenye makalio, huo si mpango wa Mungu kwa mvulana. Msichana aweza kuolewa na mtu mwenye uwezo, wewe mvulana ndiyo mtafutaji. Ni aibu kunyemelea msichana tajiri eti maisha yako yawe rahisi. Kama ni mipango ya Mungu itokee vile, basi nawe ujishughulishe na kuwa mtafutaji ili usidharauliwe na mke au wakwe zako. Kama unataka kuwa injinia, lazima usomee hesabu na sayansi kuanzia leo. Kama unataka kuwa kuhani, anza kupanga mikakati. Mungu ametuumba kuwa watendaji na si watazamaji.

Jifunze kusoma Neno la Mungu, ukiamka tu, goli si kwamba umesoma kurasa ngapi, bali mahusiano yako na Mungu. Mungu anataka kuzungumza yale ya muhimu kwako (concerns), anataka ajue ndoto zako. Mungu ana nguvu tosha za kumwamsha mwanamume au mvulana mnyonge atoke kwenye kitanda na kusoma Neno lake, mwombe akusaidie uamke na kusoma. Mwumbaji ataka awe karibu nawe, hebu mruhusu.

Mara nyingi katika maisha watu watashindwa kutuelewa. Kutoeleweka kwingine (misunderstood), kama umesingiziwa, jifunze kukaba ulimi wako na

kusema kweli tu mpaka yale uliyosingiziwa yapite. Ila kusingiziwa ni nafasi ya Mungu kutufundisha uvumilivu, unyenyekevu na kusamehe watu. Hata Bwana alisingiziwa na kusemewa uongo. Badala ya kukasirika na kushangaa, poa na umwombe BWANA nguvu. Uwe na amani moyoni, kwamba Mungu anaelewa, na kujua nia yako ya ndani. Kutenda mema ni silaha. Mwenyezi anatumia kupiga yale ambayo watu wanayotusingizia au kukupachika.

Mara nyingine hutaelewa na utachoka kusingiziwa na kueleweka visivyo, ila kumbuka tuko katika pambano kuu kati ya wema na ubaya. Shetani amemsingizia Mungu kwamba si wa haki, na wengine wameamini; ila siku moja karibuni, tabia ya Mungu itafutwa madoa machafu.

Jitahidi usiwe na nia (attitude) ya kufanya kazi ili ucheze. Wanaume wengi wanaona kwamba kazi ni njia ya kupata pesa ya kununua vitu vya kujifurahisha wachezee siku wasizo kazini. Wanaume wana michezo ( adult toys) ghali kama vile magari ghali, pikipiki ghali, boti na vingineyo. Kumbuka kwamba kufanya kazi ili kutafuta riziki ni muhimu; ila kuna kazi nyingine pia za kusaidia watu kama wajane, maskini, yatima. Hii pia ni muhimu, kuleta kupona kwa wengine. Tumia karama na ustadi wako kufanya dunia iwe mahali bora.

Ili upate mahitaji kwa hali bora, wazazi wako wanafanya kazi. Mwana mwema hatataka kuchukua kazi au mali ya wazazi wake na kutumia kwa anasa zake. Unaporithi mali, uwe mwangalifu ili usaidie wengine wa kizazi kinachofuata. Tumeokolewa kwa neema na si kwa matendo yetu, hivyo tufikirie wengine/kizazi kingine.

Je, mwana anaogopa giza, mbwa, milima mirefu, au buibui? Kuondoa woga ni sehemu ya kukua na kuwa mwanamume. Inawezekana usiondoe woga wote, bali utanawiri na kushinda mazingira yako, japokuwa una woga fulani.

Musa alikuwa na woga huo, Kutoka 3-4. Yoshua aliambiwa, 'Uwe hodari na moyo wa ushujaa, usiogope wala usifadhaike, kwa kuwa BWANA, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendapo.' Mtu anashinda woga wake kwa kujua kwamba Mwenyezi yupo, na kwamba ana uwezo. Mwenyezi anajua unachohitaji, na atakupa ujasiri na kujiamini bali si kiburi. Ushindi unakuwa na utamu endapo umeushughulikia, 'Nawaandikia nyinyi vijana kwa vile mna nguvu na mmeshinda mwovu.'

Kila mwanamume anapata woga wakati fulani, hauwezi kushinda endapo hauna maadui wa kupigana nao. Kila mwanamume ana changamoto. Cha muhimu ni kushinda mapambano madogo unayokuwa nayo ya kila siku, mapambano yaliyo ndani ya moyo wako. Kuna siku hutataka kufanya kazi, bali itabidi ufanye. Ushindi unapatikana, hasa unapochukulia hasira, ulafi, tamaa za moyo wako kama maadui zako.

Asilimia 90% ya woga tulio nao ni vitu ambavyo havitatokea. Iliyobaki 10%, utapambana nayo, na unaweza ukashindwa machache, ila ukiendelea kupambana kwa nguvu, utashinda.

Uchoyo uwe mwiko, na kama una shida hiyo, si lazima uwe hivyo maisha yako yote. Mvulana atakuwa kiongozi wa nyumba yake na hata taifa, na kupanga mipango ya kusaidia watu, endapo ni mchoyo au anayejifikiria mwenyewe, ataumiza wengi. Wengi wanaosaidia mahitaji ya watu ya taifa kwenye ustawi wa jamii ni wanaume, hivyo mvulana ajifunze kuukana uchoyo au ubinafsi.

Kina mama wanatoa kwa ukarimu chakula au vitu vichache vya nyumbani, ila wanaume wanashughulikia mipango mikubwa ya kusaidia jamii na hata nchi nzima, na wakati mwingine kukiwa na matukio ya majanga au maafa wanaokoa wengi. Twapaswa kufundisha vijana wetu kutokuwa na 'umimi.'

Kijana aombe na kuwa mwazi 'Mwenyezi Mungu, mimi nina uchoyo, najifikiria kuliko mtu mwingine. Najua hupendi niwe hivi, naomba unifungue macho yangu, nione mahitaji ya wengine ili niweze kuwa msaada. Naomba niwe na tabia kama yako.'

Piga picha baba yako anavyosikia akija nyumbani, je waweza kumsaidia kufanya jambo fulani, na mama yako waweza kumpunguzia uchovu wake? Ukimtembelea mtu angalia yale unayoweza kusaidia, badala ya kukaa kwenye kona utazamwe. Tumia muda wako kwa huduma ni msaada kwako kuondoa woga na uchoyo wa kujifikiria mwenyewe. Usiwe na haya au aibu, maumivu, au huzuni zako; anza kusaidia wengine.

Kila kiongozi mwenye njozi lazima afikirie kuhudumia watu. Watu wachoyo wanakosa ujasiri. Watu jasiri hawangoji nafasi kubwa za kuwa mashujaa au kuokoa watu, bali nafasi ndogo ndogo zinazojitokeza kila siku. Hizo zakupa nafasi ya kuwa jasiri au mwoga.

Jifunze kupenda vitu vya aina fulani. Wavulana wengi wanalalamika; 'Sipendi mvua, sipendi kazi niliyopewa, sipendi jua kali, sipendi kuishi mji huu, sipendi hichi kijiji, sipendi, sipendi sipendi!'. Kama unataka kufurahia ukuu na mema wa Mungu, jifunze kuyapenda yale aliyokuwekea wazi kuyapenda. Una uchaguzi, wa kulalamika na kunung'unika kwa kunyatisha sura, au kuvipenda vile ulivyopewa. Ila huna haja ya kuweka sura mbaya siku nzima.

Mwanamume mmoja alisema utotoni alikuwa hapendi nyanya, ila alipooa, mke wake alimpikia na nyanya. Naye akasema 'Nyanya hizi zinafanya nini kwenye chakula changu?' Lakini mke wake hakubadilisha kitu; akaanza kuzipenda na hata leo anapenda nyanya na anazimiss zisipokuwepo. Lakini twasema usipende uovu au vitu visivyo na afya, ila kuna vitu vingi waweza kujifunza kuchukuliana navyo na ukakuta unavipenda.

Wengi wamependa uyoga, au parachichi (ovacado), japo walishindwa kula vyakula hivi, walipokuwa wadogo kwa kubadilisha nia zao (attitudes). Kukomaa, na kukua ni kupenda mambo mengi yale machungu na matamu pia. Usijikaze tu 'kula nyanya' ila jifunze kuzipenda. Mungu ana mema mengi katika milki yake, tusiishi tukiepusha pua zetu kwamba 'sipendi ladha yake.' kwa vile Mungu alituruhusu tule.

Ili kuwa mwanamume kila mvulana ajifunze kuchukuliana na maumivu. Ni sehemu ya maisha ya kupata hekima, nguvu na ustadi. Mtoto asiyejikana nafsi, anapiga mayowe kwa maumivu madogo; anafikiri furaha yake zaidi ya majukumu yake. Badala ya kufanya kazi shambani anafikiria jinsi jua lilivyo kali, au kuchoka kwake. Badala ya kumpisha kiti mama mzee, anafikiria raha au burudani yake. Akijikwaruza mkono kidogo, anakataa kuosha vyombo. Maisha yana maumivu mengi zaidi ya mikwaruzo midogo. Uumbaji wote unalalamika na maumivu ya aina fulani yawe ya kiroho, kimwili au kiakili. Hata wengi wana maumivu kwa mtu kusema maneno yasiyo ya upole, siyo tu kwamba wewe ndiye unayelengwa! Hivyo usijionee huruma ukiumia, kwa sababu kila kiumbe kinapata maumivu. Mwanamume apaswa kujua jinsi ya kuchukuliana na maumivu, hawezi kujificha. Bila maumivu mara nyingine hakuna matunda au maendeleo.

Maumivu ni ya wote, na mara nyingi ni ya muda mfupi. Ila mbinguni hakuna maumivu, yale yanayotuumiza leo, yaweza kuisha kesho, hivyo usikite kwenye maumivu yako. Maumivu pia yana mwisho wake, ingawa kuna wakati tunaona tunashindwa kustahimili. Maumivu hayako huru kutufanyia yatakavyo kwani Mwenyezi anamiliki na kujua mwisho wa uvumilivu wetu, hivyo anatupa tu yale tunayoweza kuyastahimili. Mungu anajua kila urefu na uzito wa kila umivu, na ametoa ruhusa lije kwetu; 1Wak 10:13. Kama kisa cha Ayubu kinavyosema, hakuruhusu Ayubu kufikia anaposhindwa kustahimili. Maumivu yana uzuri fulani, Mungu hawezi kutupa bila sababu.

Mtu wa karibu nasi, anapotuumiza mioyo yetu kwa kutotuelewa au kwa mategemeo yetu kutotimizwa inatuumiza zaidi ya kawaida. Daudi alisema 'Kwa maana aliyetukana si wa mbali; kama ndivyo, ningevumilia. Aliyejitukuza juu yangu siye anichukiaye; kama ndivyo, angejificha asinione. Bali ni wewe, mtu mwenzangu, rafiki yangu niliyejuana nawe sana. Tulipeana shauri tamu; na kutembea nyumbani mwa Mungu pamoja na mkutano.'

Jinsi unavyojibu watu wanaokuudhi na kukwambia maneno ya kukuumiza, inaonyesha kama unakomaa kuwa mtu wa Mungu au unajifikiria wewe na maumivu yako tu. Mlilie Mungu ili akuliwaze, na usipige mayowe kwa muda mrefu kwa maumivu madogo, au kukasirika kama mambo hayakuendei unavyotaka.

Watu wengi wanapenda kuepuka maumivu ila wachache kati ya hawa wanafaa kwa ufalme wa Mungu. Ukiwa na maumivu au vidonda vya mwili, nenda hospitali ukashonwe, au kurudishwa mfupa sawa, ila usionyeshe kidonda chako kwa kila mtu.

Mwanamume lazima awe shujaa, asiyetaka huruma (pity) toka kwa kila mtu. Badala ya kuangalia kidonda chako kila wakati, angalia watu wa kuhudumia, ila utoe mawazo yako kutoka kwako na maumivu yako. Kwa maumivu ya moyo, usiwe kama mbwa anayelamba vidonda vyake siku nzima, ila 'ushinde wema kwa ubaya.' Hata Bwana 'Kwa ajili ya furaha iliyowekewa mbele yake, aliustahimili

msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu.'

Kuna wakati wa kutoa machozi, na kucheka. Siamini msemo kwamba 'mwanamume halii,' kwani hata Bwana Alilia; ila hakulia kwa huzuni zake ila za watu wengine. Kulia kunapunguza maumivu ya moyo. Hivyo kuna wakati wa kujikaza, na kuna wakati wa kulia, na hiyo Bwana atawawezesha wana kutofautisha, ili wasiwe watu wa kulia lia ovyo, au kutolia na kupata shida za hisia.

Unawezaje kujitayarisha kuishi na mke vizuri sasa? Waweza kufikiri u mdogo bado, kufikiri hili na ukacheka, na ni kweli si wakati wa kuoa, ila waweza kujitayarisha wakati huu. Waweza kujitayarisha kimawazo sasa, ili baadaye uwe mwanamume wa furaha na kuwa na ndoa ya furaha. Siyo kwamba unaharakisha kuoa, ila ni bora uwe tayari hata kama hautaoa au ukipata wito wa kuwa towashi. Jifunze kazi ambazo wanaume wanasaidia dada zao, au mama zao; kama vile kubadilisha tairi, kukarabati nyumba, kuzibua choo, kuweka mbolea, kufuga nyuki, kuchunga mifugo, kutoa visiki, kutumia nyundo na bisi bisi, kutengeneza zizi, kuchagua mbegu za kupanda, kuua panya au kupunguza matawi ya miti ya matunda.

Jinsi unavyowahudumia dada zako na mama yako sasa ndiyo darasa kubwa la ndoa. Wadogo zako wafurahi wana kaka mkubwa, wakupende, nawe uwapende pia. Jinsi ya kujenga mahusiano bora na dada au mama yako ndiyo jinsi ya kujenga mahusiano bora na mke wako pia. Usiwe jeuri, hata dada zako wakakuogopa na kutokwambia yaliyo moyoni mwao. Uwe na upole, ili wakuamini, na wakikuambia shida zao, chukua hiyo changamoto ya kuwatatulia bila kutangaza tangaza au kujisifu.

Je, wanapenda nini, au hawapendi nini? Je, unajua njozi zao na woga au mashaka waliyonayo? Je wana mategemeo au matumaini gani ya leo au kesho? Ukiwa jeuri na mkatili, watakuficha. Kama dada yako alitaka kupata chombo cha muziki ajifunze, chukua changamoto hii na kumsaidia akipate.

Dada yako ndiyo darasa la kukufundisha jinsi ya kutafuta riziki ya familia yako siku za mbele.

Ujasiri wa Daudi kumshinda Goliathi, haukuja siku hiyo hiyo; bali alianza kumpiga simba na dubu kwanza, ndipo akatoa woga na kuliendea jitu la kifilisti. Wahudumie madada na mama zako. Usiwe unawakejeli, kuwadhililisha, au kushindana nao kwamba wewe ndiye kijana au mwenye nguvu. Uwe timu moja nao, ikiwa chakula acha wao wapate sehemu kubwa nawe uchukue ndogo. Wape nafasi nzuri ya kukaa.

Je, umefikiria kuwaambia dada zako au nduguzo wadogo msome pamoja nao neno la Mungu? Je, unaomba nao? Wasifu wakifanya mema, na wakifanya mabaya wasamehe, wasaidie wafanye vyema na kufunika makosa yao. Una nafasi ya kuwafanya wawe warembo nje na ndani ya moyo pia. Siku moja watasema, 'Kaka yangu alinipa nafasi ya kufikia njozi zangu, nampenda na kumheshimu.'

Mdogo, dada au mama yako akiwa wa kujifikiria na mchoyo msaidie. Mwombe Mungu akusaidie, na kazi yako itakuwa ni kurudisha mahusiano mema. Nawe pia uwe mfano kwa wadogo zako, dada na mama. Bwana amefanya mamilioni wasiompenda wampende, nawe fanya vile. Mvulana aliyekomaa haangalii nani anampenda na nani hampendi, bali anaangalia kufanya vyema bila kujali watu wanavyomtendea. Usifikirie wadogo zako, dada au mama hawataki uwasaidie na kuwapenda. Mara nyingi watabadilika. Wasichana wana kigeugeu wakati mwingine; ila wewe tafuta njia za kuwapendeza dada zako, mwulize hata mama yako, atakusaidia. Ni kazi ya mvulana na mwanamume kuwapendeza dada zake na hatimaye, mke wake.

Unapochagua mke, mpe Mungu nafasi ya kukuchagulia, omba na ungoje wakati atakaokuchagulia. Mtu anachagua anayoona nje, ila BWANA anajua moyo. Angalia kama anapenda mambo ya kiroho. Epuka michezo rafu unayocheza na wanaume. Iwe mwiko kudansi na wasichana, maana inaamsha tamaa mbovu. Mashule mengi ya bweni yanaweka dansi na yamewaingiza vijana kwenye tamaa na dhambi. Kila siku tuna mapambano vichwani mwetu, na falme ya shetani. Vaa mavazi ya vita ya waefeso 6, usijianike kwenye majaribu.

Dansi ni chombo cha shetani mwenyewe. Mwulize mwanamume yoyote kama atakubali mtu acheze dansi na mke wake wakikumbatiana, atakwambia la! Zama zile za ukoloni, watu walikatazwa kucheza ngoma za kienyeji eti ni za kishenzi, cha ajabu ni kwamba ngoma hizi watu walicheza mbali na mwingine, mwanaume na msichana hawakuwa karibu. Siku hizi dhambi zafanyika kwa wazi, za kukumbatia msichana asiye mke kwa karibu.

Wengi wanafundishwa mambo ya kuvaa kondomu, ila kwa mtu anayemweheshimu Mungu. Ngono ni ya ndani ya ndoa tu, nje ya hapo ni dhambi au uasi wa sheria za Mungu . Hata hivyo kondomu haifuti dhambi, haindoi dhamira kushitaki, haizuii mimba au ukimwi kikamilifu au  kutoa huzuni.

Mtoto wa kiume daima ajue kwamba ni Mungu pekee ndiye msaada wa kuepuka dhambi za ngono. Wanaume wengi hasa katika ulimwengu wa leo wa ponografia (umalaya wa picha) wameangushwa au kuingia dhambini kwa mambo matatu yaani wanawake, pesa na kiburi cha mamlaka (power). Kama mvulana au mwanamume anajiona yeye hawezi kuanguka mtego huo, basi lazima atakuwa na nguvu kumpita Samsoni, Hekima za kumpita Sulemani na kumpenda Mungu hata kumpita Daudi.

'Apataye mke apata kitu chema na kupata ijara toka kwa BWANA.' Mvulana atofautishe kati ya mwanamke mgeni wa  Mithali 7; yaani malaya na mwanamke bora wa Mithali 31. Je, ana tabia kamili za msichana bora?  Je, anajua tendo la ndoa katika Neno la Mungu lina sehemu gani? Mfundishe mabadiliko ya mwili kama vile kubalehe, na endelea kuzungumza naye katika kila hatua.

Wazazi wengi wazungumza na watoto wakiwa na miaka kumi na mitatu na kuachia pale; kisha wanashtuka mambo yakiharibika wakiwa na miaka kumi na

saba! Kumbe walitoa somo moja tu la ngono na kuacha! Majaribu ya ngono yanafikia wengi na punyeto; mtoto afundishwe kuepuka haya kila mara. Watenge watoto wako wasilale na watu wengine, na mambo ya sherehe za usiku (pajama party au sleep over) yawe mwiko.

Mvulana kujiweka safi kwa maneno, mawazo na mwili mpaka aoe. Je, ana mpango wa kumwendea baba wa msichana kabla ya kufungua ndoa na si kukaa pamoja bila mipango ya ndoa? (come we stay). Je, yupo tayari kukwambia anapotaka kuoa? Je, yupo tayari kukaa msela endapo Mungu amemwita kuwa towashi, na kutoishi maisha ya ndumila kuwili?

Biblia si kitabu cha ushauri bora au maoni bora tu, bali mawazo ya Mungu mwenyewe, yenye mamlaka ya mwisho mbinguni na duniani. Neno la Bwana latueleza jinsi ya kuchukuliana na kumpendeza kila mtu unayekutana naye, awe rafiki, dada, kaka, wazazi, mwajiri, wasichana, wazee , maadui au watoto. Inawapa watu tahadhari na mitego, inakueleza jinsi ya kufanya kazi, kuwekeza pesa, jinsi ya kula, cha kula, na hata wakati wa kulala. Ina kanuni za kila nyanja ya maisha yako. Inatupa kina cha kujua Mungu anavyofanya kazi na kusikia sauti yake. Inafanya tujue maisha, mambo ya asili na hata ya sayari nyingine. Inatueleza kuanzia Mwanzo mpaka ufunuo jinsi ya kumpokea BWANA aliyejitoa kwa ajili yetu kwa kutupa uzima wa milele.

Wewe siyo mnyama kama elimu ya uibukaji inavyopoteza, umeumbwa kwa makusudi maalumu. Kila mvulana ajiulize yupo hapa kwa ajili gani, ametoka wapi, na nini kitatokea akifa. Neno la Mungu laeleza kwa nini kuna maumivu haya yote. Hakuna kitabu chochote kitakueleza yote haya. Saa moja kwenye kitabu kingine kamwe haitalingana na saa moja kwenye Neno lake.

Hakuna kitabu cha kusisimua kama hiki, na kinachobadilisha maisha ya mtu. Hesabu au kemia haiwezi kubadilisha maisha yako kama kitabu hiki. Ila Biblia si kitabu cha kupata habari bali kubadilisha maisha (not for information but transformation). Ukifuata ushauri wako, mambo yatakuwa halisi na utabadilishwa. Usipoteze muda kusoma hadithi za nadharia (novel) au fictions ambazo zinafanya usipende kusoma Neno la Mungu. Hadithi za kufikirika zafanya Biblia isiwe na ladha.

Akili zako zitapanuka, ukisoma Neno hili na hata utakuwa na uwezo mkubwa darasani. Soma na elezea marafiki, ulichopata kwenye sura hiyo. Wakati mwingine unyamaze kwa utulivu na kuangalia Utukufu wake. Kariri mafungu yake mengi, imba nyimbo. Marko 1:35 inasema, 'Alitoka kwa faragha aende kusali;' nawe, amka na ukasali.

Sikiliza mausia ya wazee, hautakuwa kama rika lako bali utakuwa na hekima ya kupita umri wako. Mashauri haya ya wazee yanaweza kuonekana yamepitwa na wakati, ila utakuwa unatafuna mambo na kucheua kwa hekima ambayo watoto wa umri wako hawana. Twaona Sulemani alipokufa kijana wake Rehoboamu aliomba ushauri kwa vijana wakampotosha, naye akapoteza ufalme wake.

Wazee wenye hekima hawazungumzi mawazo yao kwa haraka, wanapima mambo kwanza. Wanajua maisha ya mvulana au mtoto yatakuwaje, hata kama hawakwenda shule; kwani miaka ya uzoefu waliyonayo inawasaidia. Wengi wamepinga ushauri wao, na hii imewafanya wanyamaze, wakiogopa kujichumia uadui na vijana. Hivyo ni jukumu la wavulana na vijana kukaa na wazee na kuwauliza maswali ya taaluma nzuri ya kusomea au ustadi gani ni wa muhimu kupata, au uwekezaji gani bora, n.k.

Mpepeleze mzee kwa maswali kama haya: Je, mtu afanye yapi kuwa na mahusiano mazuri? Je, mambo gani yanaharibu mahusiano? Je, jamii imebadilika kwa namna gani leo? Je, imebadilika kwa mazuri au mabaya gani? Ni makosa yapi uliyoyafanya mambo yakaharibika? Ni sehemu gani ya maisha yako mambo yalikuendea vizuri sana? Nini waweza kunielemisha kuhusu ndoa na kuwa na watoto? Ukiwa mwajiri, ni mtu gani utamchukua kwenye kampuni yako? Ukiwa mdogo wakumbuka ushauri aliokupa baba yako? Je, uliufuata? Je, ni nini kilicho muhimu sasa kwenye maisha yako? Je, upo tayari kufa wakati wowote? Kama ndiyo! kwanini? Kama la! Kwanini?

Kuna wakati wa kuua na wakati wa kuponya (Mhubiri 3), na hiyo ni changamoto ya kukua au kuwa mwanamume. Watu wengi wanachanganyikiwa na kuua wakati wasipopaswa na kutoua wanapopaswa. Je, mvulana atajuaje? Mwanamume au mvulana si mnyama mwingine kwenye himaya ya Mungu. Alipewa mamlaka na milki. Anapaswa kuheshimu viumbe na kuwa wakili bora, si kuua viumbe au kukata miti bila sababu, eti alimradi iko kwenye milki yake. Anapaswa kuvitumia hivi vitu kwa mahitaji yake, ila si kwa ufujaji, akikata miti apande miti. Asiwe mkatili, ajue kuhifadhi, pia ni kitu gani atakachokihifadhi. Mfano, panya wako katika nyumba wanakula mahindi yako, Je, uwaue? Siafu walio porini uwaue? Je, paka anayekatisha barabara umuue? Ukiwa unaishi karibu na mbuga ya wanyama na una njaa, je, uue swala bila kibali? Usipuuzie kazi ambayo Mungu alikupatia, ya kuhifadhi na kujali viumbe. Hata wanyama wanajua ni nani anamcha Mwenyezi Mungu kutokana na huruma na utunzaji wanyama anaofanya huyo mtu. Je, mifugo yako inapewa malisho au chakula na kushiba? Au unafuga mbwa bila kumpa chakula mpaka mbavu zake zinaonekana? Kumbuka Nuhu aliambiwa aweke wanyama kwenye safina, Mungu aliweza kuwaumba wengine, ila aliwapenda wale wanyama. Biblia yasema Mungu akamkumbuka Nuhu na wanyama.

Ili mtu akidhi mahitaji ya familia yake kiriziki anahitaji kuua mara nyingine, ila asiue viumbe vya Mungu kwa ajili ya hasira au futuhi bali kwa riziki au ulinzi. Wakati vita vimetokea, tunajua wazi kwamba watu wengi wanaompenda Mwenyezi Mungu wamepigana vita vya kuleta uhuru na kulinda nchi zetu au jumuiya. Wengine kutokana na dhamira na sehemu Mungu amewapa kufanya, wamekataa kuua kwenye vita na kushughulikia majeruhi wa vita na hiyo ni sawa kutokana na mtu na kuelewa mambo fulani. Ila wanaume wote lazima wajue jinsi ya kulinda familia zao na kujua kuleta riziki.

Mwanadamu ana jukumu la kutunza hifadhi za karibu na kwake na kutokuwa mharibifu. Wavulana wengine wamepiga ndege kwa manati na kucheka tu bila sababu yoyote ya maana. Mwanamume anahitaji kutunza vile Mungu amemkabidhi, yakiwemo mazingira. Tunaishi wakati ambao watu wanaua hata watoto wao wenyewe kwa kutoa mimba au njia zingine. Watu wako tayari kuua watoto wao ila wanaogopa kuua mende kwenye makabati yao. Lazima tujue thamani ya binadamu, na wakati huo huo kuwa na ujasiri wa kuua vitu kama mende au panya.

Ibada ya nyumban ni muhimu. Usikunje ndita wakati wa maombi au ibada. Waisraeli walichukua muda mwingi wa ibada, na kutoa kafara, ila walikuwa na kujifikiria na uchoyo. Kila siku ni siku ya ibada, pia kwa jinsi tunavyoishi tunaabudu. Maana twaweza kuwa waimbaji wazuri ila maisha yetu yana harufu mbaya. Twahitaji mioyo yetu kubadilika, ili tusiwe na vichwa vilivyojaa neno la Mungu bali mioyo iliyojaa dhambi.

Kama unataka kuwa mwanamume kweli ambaye Mungu atamtumia, jifunze kumwabudu Mungu jinsi anavyotaka kuabudiwa. Mwabudu kila siku katika uzuri na Utakatifu wake. Mahusiano na mawasiliano ni muhimu. Jifunze kuandika barua za kutia watu moyo. Jifunze kuandika barua rahisi, na unapoendelea kuandika utakuwa na ustadi huo, na utakuwa na barua nzuri. Wengi wanapata barua za kulalamikiwa, na watakapoona barua ya kushukuriwa, watashangaa na kupata ujasiri na watatunza barua yako milele.

Ninapoishi, watu wengi wanaogopa kupokea zawadi kwa ajili ya kujisikia wana deni, kiburi au hawataki kuwa kwenye 'mgawo wa ustawi wa jamii.' Wengine wanaogopa kuandika barua za kushukuru. Kutoa na kupokea zawadi kunajenga mahusiano mazuri. Ukiacha kupokea zawadi watu watafikiri kwamba wewe unaona vitu vyako ndiyo vya maana, au hutaki kutoa vyako na hivyo, unawafungia mlango. Kutoa ni mbaraka kuliko kupokea hivyo usifanye watu wengine wapoteze bara zao kwa kutopokea vyao, wakikupa kitu kwa nia nzuri.

Kwa watoto wetu, tunawapa mazoezi ya kutoa tukipokea pia. Ila andika barua ya kuwashukuru na ukilenga kile unachoshukuru; mfano: 'Asante kwa hela, zimenisaidia sana msimu huu kwa kilimo cha matango.' Wengi waandika barua kuomba vitu wakiwa wanafunzi shuleni (boarding), bali wakiwa watu wazima na hawahitaji kitu, hawaandiki ng'o; hili ni kosa. Mawasilianosi kwa kupata vitu bali huduma ya upendo.

Twajitayarishaje kuwa baba bora tukiwa vijana wadogo? Jibu: Kwa kufanya vile ambavyo tungetaka watoto wetu wawe! Usifikiri jinsi utakavyowalea watoto wako, bali fikiri vile Mungu anataka uwe kama Yeye. Watoto wako wakiwa rika lako, Je, wataka wawe wa tabia gani? Maana watoto wako watataka kuwa kama wewe. Je, wewe ni mwaminifu? Je, ni mtenda kazi mwema? Je, wapenda kunung'unika kila mara? Fahamu kwamba watafuata mfano wako.

Mungu ana huruma, japokuwa umeharibu mambo. Maana hatupi tunayostahili (exceptions). Si tabia zako zote mbovu zitaelekea kwa watoto wako bali 'tunda halianguki mbali na mti.' Watoto utakaozaa watafanana na wewe. Mvulana wako akiwa na miaka kumi na miwili atakuwa kama wewe ulivyokuwa miaka na miaka kumi na miwili. Kama u mvulana mwenye shukrani, na mwenye bidii naye atakuwa vile vile, ila kama u mvivu atarithi tabia hiyo mbovu. Ukiwa na bidii ya mazoezi ya chombo cha muziki, naye atakua vile. Somo lolote utakalofanyia bidii naye pia atalifanyia, unachofurahia nao watafurahia. Mfano wako utawafundisha mno.

Tabia ya leo itakufanya uwe mwanamume wa kesho, na hiyo itaathiri watoto wako. Waweza kufikiri mimi ni mtoto tu, nitashughulikia hili au lile nikiwa mtu mzima. Utashangaa siku zimefika, na u mtu mzima na kufanya tu yale uliyoyafanya ukiwa mtoto! Hivyo anza leo kubadilisha mwenendo, una nafasi ndogo ya kubadilisha mwenendo kesho.

Uwe na njozi ya kufanya vitu kama mwanamume, na njozi hizi za hekima na maarifa zitakusaidia uwe na mahusiano mazuri na utajiri wa kikweli (true wealth). Kila siku ujenga matofali ya tabia ambayo inakuwa ngumu kama simenti, ikiwa mbaya ni kazi kuiondoa kizazi kinachokuja.

Tabia njema ni kama kuweka akiba kwenye akaunti ya watoto wako. Ukielewa somo, utaepuka mashimo mengi, wavulana waweza kubadilisha mambo kirahisi kuliko wanaume wazee. Angalia maisha yako kwa uaminifu na uyakague vizuri, waulize marafiki au wazazi wako udhaifu wako na uzuri wako. Mwombe Mwenyezi akufanye wewe uwe mwanamume ambaye unafaa, kisha uanze kubadilisha mwenendo leo.

Je, mwana aweza kuongoza maombi na kusoma Neno la Mungu na kuneemeka? Je, aweza kugawa mamlaka hata kwa ndugu zake wafanye? Lazima kuwe na ratiba ya kufanya kazi kwa watoto wote nyumbani.

Kusaidia vilema na kutowacheka au kuwakejeli ni muhimu. Ninapoishi, mtu mmoja wa Afrika mashariki pamoja na mkewe, walikuwa wakicheka vilema wenye vichwa vikubwa na utindio wa ubongo, walipofanyia kazi. Walipofunga ndoa na kupata mtoto wa kwanza alikuwa na kilema kigumu cha kukosa njia yote ya mkojo, Ilibidi waishi hospitalini. Watu walisema, 'sasa hawana haja ya kucheka mbali, wana cha kucheka karibu, nyumbani mwao!' Walinyenyekea na kuwa watu wanaoelewa shida za watu. Ni kweli mara zingine tunapata shida ya ulema hata kama hatukucheka, maana mapenzi na utukufu wa Mungu hatujui, lakini tunapocheka shida za watu dhamira hutushitaki. www.truthforyourfamily.org by Joel Beeke.

Ukitaka kuwa mtu mcheshi mwenye bidii, watoto wako watakuwa vile pia. Watapenda kazi kama baba na kuwa wacheshi. Utasema, inakuwaje nami ni

mvulana hivyo hawanioni sasa? Mpango wa Mungu wa kuishi, kwamba mti mzuri unatoa matunda mema, si kwa kubahatisha tu, bali ni sheria ya mbinguni.

Je, mtoto anajua maana ya uovu ni nini? Anajua amri kumi kwamba ndiyo kipimo cha haki? Je, anajua rehema za Mungu na kutendea watu kwa haki au ana ubaguzi? Maana Mungu anataka tuenende kwa haki, rehema na unyenyekevu. Je, aweza kuwakanya ndugu zake? Je, anapata hasira na kuwakasirikia ndugu zake? Je, hapendi kusahihishwa? Apaswa kujua kusimamia nyumba yake vizuri? Watoto wapewe kazi kutokana na umri, mfano kusafisha gari, kukata majani, kulima shamba, n.k.

Kukana nafsi ni muhimu kwani bustani ya Edeni ilipotea kwa kutotawala tamaa ya chakula, na ulafi. Mtoto afundishwe kuepuka hali hii. Kulinda moyo wake na mafikira kwa kutoangalia vya kuangusha kama Televisheni na compyuta zenye programu mbovu.

Aepuke kuingia kwenye madeni. Zungumzieni mambo ya madeni na jinsi ya kuepuka. Hasa siku hizi za credit cards. Alipe ikiwezekana na ajifunze kutoa sadaka na zaka. Asiwe mtu mwenye hasira, 'Asiyetawala roho yake ni mfano wa mji uliobomolewa, usio na kuta;' Mithali 25:28. Hata mtoto mdogo afundishwe kungoja bila kuwa na hasira, anapocheza na wengine.

Hasira zisizoweza kumilikiwa zinaweza kuumiza mke au watoto au mtoto wa kiume mwenyewe. Akiwa anashindwa kutawala nafsi, na kuwa na harara mfundishe 'kutojisumbua kwa neno lolote, bali katika kusali na kuomba akishukuru aweke haja zake kwa Mungu, na amani ipitayo akili itamhifadhi kwa moyo na nia.' Akiendelea kufikiri yote ya kweli, ya haki, safi, yenye kupendeza, yaliyo na staha, mema, na sifa nzuri, na kutafakari hayo.

Ajifunze jinsi ya kuhudumia familia, na kuwa na adabu njema (manners), maana hizi haziji zenyewe bila kuzifanyia mazoezi. Ajifunze kusema samahani, pole , asante, tafadhali, nisamehe, naomba. Ajifunze kutonyanyasa watu walio chini yake, maana watoto wengi walionyanyaswa na wazazi wao huendeleza tabia hiyo, ila aende mbele za Mungu, kuzikanusha nguvu hizo, au laana hiyo ikatike katika kizazi chake, ili isiendelee kizazi cha tatu na cha nne.

Je, ana muda mwingi wa kupoteza na kukaa kwenye TV. Je, anajifunza tabia za kuwa mtu wa bidii? Je, waweza kumtegemea akufanyie kazi fulani bila kupeleka mawazo yake kwenye vyombo vya teknolojia? Je, marafiki zake wa karibu wanampenda Mungu au apenda kujiegesha na watu waovu kama Delila? Je, anajua jinsi ya kuwa na urafiki wa kawaida na wasichana bila kujiingiza kwenye urafiki mbaya? Je, ni tabia gani za kuepuka kwa marafiki?

Je, anatoa udhuru wa kuhudhuria ibada? Je, kila saa anatoka kunywa maji au kwenda chooni wakati wa ibada? Je, anamtegemea Mungu au ananung'unika mambo yasipoenda vizuri? Je, anaweza kumaliza kazi uliyompa kama vile Nuhu au Nehemia? Je anaweza kutimiza ahadi zake kama vile Elkana na mke wake? Au

mawazo yake yanatawanyika huku na kule? Je, vitu vyake aviacha kila mahali? Hata akivua nguo suruali yake inasimama kwenye sakafu pale pale alivulia?

Mara zingine wazazi wanahusika na kuhudumia watu, na mtoto anapata attention ambayo wazazi hawajui. Hili nilijifunza kwa mhubiri Billy Graham, alipokuwa mashuhuri sana, watoto wake walikaa karibu na lango (gate) la nyumba na kabla wale watu kumtembelea mhubiri, wale watoto waliwaomba washiriki pesa au vitu. Wageni waliona aibu kwaajili ya baba yao wakawapa hawa watoto vile vitu, bila ya kuripoti kwake. Tabia hii alikuwa nayo Gehazi mtumishi wa Elisha! Aliomba nguo mbili na visenti na kupaka matope kazi kubwa ya nabii. Mhubiri huyu alikuja kugundua baadaye, kama wewe mzazi u mashuhuri au wahusika na mambo fulani ambayo watu wengi wakujia, angalia watoto jinsi wanavyohusika na watu, ili uwaepushe na uovu wa namna fulani.

Je, anaweza kuwa mkarimu kama Ibrahimu kukaribisha watu asiowajua na kupata mibaraka? Soma kuhusu ukarimu na kukaribisha wageni. Je, anajua ukarimu kwa familia yake pia? Je anaogopa kupokea simu, kujibu barua au kufungulia wageni milango? 'tazama nabisha mlangoni. Yawezekana Yesu akabisha mlango. Siku hizi pengine hatupati wageni nyumbani ila hata simu zetu mara zingine ni watu wanaohitaji ushauri au huduma kutoka kwetu. Nimejifunza mara nyingi pia ni watu ambao wananibariki mimi, na si mimi nawabariki, kama vile Abrahamu, mgeni yule alimbariki, na si Abrahamu alimbariki yule mgeni! Mwana ajifunze kuwa mhudumu, si kuepuka wageni

Basi mtoto wa kiume asiyejua kutafuta riziki, ni mwovu zaidi ya yule asiye muumini. Japokuwa wanawake wanajitafutia riziki wenyewe siku hizi, hili ni jukumu la kwanza la mwanamume. Hii inataka mwanamume asiwe mbinafsi, na wazazi tuwasaidie watoto wetu wa kiume waweze kuwa watafutaji kwa njia halali. Wasaidie wadogo zao, babu na bibi na pia miradi ya familia. Zungumzeni bajeti ya familia, na jinsi wanavyoweza kutafuta vibarua vidogo vidogo.

Je, aweza kujitafutia mahari yake mwenyewe? Je, anajua jukumu la kutunza wazazi waliozeeka? Je, anasaidia kazi za nyumbani kwa uaminifu? Je, ana ukarimu wa kusaidia wenye mahitaji na kumwonyesha jinsi ya kufanya? Ajifunze kuwa msikilizaji mzuri, na kutoingilia mazungumzo ya watu wengine

Je, anakumbuka kuwaombea wengine au huwa anajifikiria na kuleta shida zake tu mbele za Mungu? (intercessory)? Je, anajua kuungama dhambi akikosa? Je, anajua kusimulia kisa cha wokovu kwa dakika chache, akielezea mafungu yake?

Je, anataka kuoa binti wa namna gani? Je, anawaheshimu wasichana kama ni wake za watu wa siku za usoni na hivyo anawakinga na uovu, na uchafu ili wawe mabikira kwa waume zao baadaye?

Mara nyingi tumejaribu tunavyoweza, hapo tunamwachia Mungu ndiye MWEZA. Hatuwezi kujua kwa nini jambo fulani limetendeka kwetu, ila matukio mengi tunaweza kujua mwishowe yana mshahara gani.

Mvulana atakayeishi kutokana na hukumu na sheria za Mungu atavuna matunda ya watoto wanaompenda Mungu siku za usoni. Mithali 22:6. Hivyo unapojaribiwa kufanya uovu au upumbavu fulani, kama kuvunja sheria, fikiria maamuzi yako, na kwamba yatajirudia kizazi kijacho, hata cha tatu na cha nne. Hivyo ghairi ukanuie kuishi kwa msingi bora wa vizazi vijavyo. Utaishi bila majuto, na itakuwa ngome kwa watoto na wajukuu wako, Mungu atakapokujalia. Tukumbuke Mungu ni mvumilivu, mwingi wa rehema, na anasamehe uovu.

Je, mwana anapasa kuwa na uhusiano gani na kileo?jibu ni 'Asijaribu kuweka mdomoni, hata tone la pombe;, asivae hata tshirts zenye matangazo ya pombe au kileo au kusikiliza matangazo ya biashara ya namna hiyo. Asiende mahali ambapo kileo kinapouzwa au kumcheka mtu aliyelewa maana dhambi ni kitu cha huzuni. Kataa kutoa sababu kwamba ni lazima unywe, hata kama huna mpango wa kunywa, jua ni jaribu linaloweza kukujia, kwani wengi hawakufikiri wataingia katika ulevi. Waambie marafiki zako kwa upendo kwamba hutakunywa na sababu unamheshimu Mwenyezi Mungu. Mithali 23:32 yasema, 'Ukae mbali nayo kama unavyoweza kukaa mbali na nyoka.': 40% ya wanywaji hawawezi kuacha (alcoholic). Je Ukiwa na mbwa anayeuma watu 2 kati ya tano wanaokuja kwako utaendelea kumfuga?

Mwana ajue kwa nini anapata adhabu au masahihisho ya tabia yake ili aongozwe katika njia njema ya hekima. Mwana anayependa wazazi wake atawashukuru pale wanapomsaidia. Ajiepushe kuharibiwa na misukumo ya rika ndiyo ilimponza Samsoni. Kumpenda Mungu na kutembea katika njia zake na kumtumikia kwa mioyo, akili, nguvu na roho zetu ndiyo hekima. Maneno yake yawe yametiwa munyu ili ajue kujibu watu maana maneno yanaonyesha tabia na kile kimeujaza moyo wake. Usafi wa mawazo, maneno, na matendo (purity) ni muhimu.

## SURA YA 43

## Kukuza mtoto wa kike awe mwanamke wa mithali 31-Mafunzo kwa mama na binti.

Daudi, mwandishi wa Zaburi, azungumza maneno ya baraka kwenye Zaburi 144:11-15. "Wana wetu wawe kama miche waliokua ujanani, na binti zetu kama nguzo pembeni zilizonakshiwa na kupamba hekalu...".

Bila shaka kukuza mabinti zetu mpaka utu uzima wakiwa wanampendeza Mungu ni baraka kubwa. Wazazi wengi kwa kuwa na shughuli nyingi, wanajaribiwa kuacha watoto wajikuze wenyewe. Mungu hakutupa watoto tuwatelekeze (neglect). Uzazi ni jukumu zito, kuliko wengi tunavyofikiri. Kina mama hatuwezi kuacha watoto wetu, hata wa sekondari, wakiwa ndani ya nyumba peke yao, na sisi tuko busy, au tunasafiri kila wakati.

Wengine twafanya kazi kwa shift, wengine twajitembeza hapa na pale, na tunaacha watoto peke yao; hili ni kosa. Mawazo ya mtoto yanatembea huku na

kule wakati mwingi. Aweza kwenda kwa majirani, au kuangalia mambo yasiyofaa n.k. Wanaweza kuanza kufanya maovu, ila usiwe wewe ndiye uliyetoa nyufa. Wengine wamepeleka watoto wadogo magharibi wakawaacha huko wenyewe, bila wao kuwepo. Wengi walishindwa kumaliza shule, bali la kuhuzunisha zaidi, ni kwamba wengi waliacha imani. Waliingia kwenye ndoa za ajabu ili kupata vibali vya kazi, na kupigana na wenyeji wa nchi hizo, na wengine wakawa hoi, kwa michoko. Sulemani asema mtoto ana ujinga wa namna fulani.

Masomo ya chuoni au kwenda Magharibi yamekuwa kama miungu fulani siku hizi za mwisho. Maisha ya kumcha Mungu ni mpando. Usiache mtoto wako kwa mtu akuangalilie kama siyo dharura, kwani utamlaumu huyo mtu. Watoto wana mambo mengi; hata kama ni mtu mwema umempa hiyo shughuli. Hata hivyo ana uchungu gani na mtoto wako zaidi ya wewe?

Tulikutana na msichana mkubwa wa sekondari, aliyelelewa mbali na wazazi wake, ambaye hakusalimia watu, hakushukuru watu walipomtendea mema, wala hakufungua mdomo wake aliposalimiwa au kuulizwa maswali ya kawaida. Tulidhani ni bubu au kiziwi, bali tuligundua ni tabia alivyokuzwa bila kufundishwa adabu, au kutofahamu, (ignorance). Wengine wakasema ni 'mtu wa haya'. Haya na kukosa adabu ni vitu tofauti.

Mabinti wetu wanahitaji mafunzo (training), kwani siku za usoni watakuwa walimu wa watoto wao na watahitaji mawasiliano bora na waume zao na hata wakwe. Je, unaweza kumkanyaga mtu kwa bahati mbaya na kutotoa hata samahani?. Hata hivyo ye yote anayetaka kuwa raia wa ufalme, lazima ajue kuwaambia watu habari njema! Je atanyamaza kimya, eti anaona aibu?

Mithali 31 ina mengi ya kusema kuhusu mwanamke anavyopaswa kuwa. Nafikiri jambo hili linaanzia katika matunzo udogoni, na si ukubwani. Wengi wamesema mwanamke wa mithali 31 ni muunganiko wa wanawake wengi! Tunaona ana watu wa kumsaidia kazi zake, ila ni yeye anabidi kupangilia mipango ya mambo ya kufanya. Kama wazazi na hasa kwa wanawake, tuna haja ya kujifunza zaidi kuhusu mwanamke wa Mithali 31 kwa undani. Maswali haya na majibu ni kwa mjadala na mabinti zetu. Tuendele kuwaongoza na kuwathathmini, nasi wenyewe tutazidi kukua katika safari ya kwenda mbinguni.

Mama Pam Foster wa doorpost.org amemzungumzia mwanamke huyu kwa undani. Tumechukua maswali yake, nawe utachukua nafasi kila siku kujadili na binti yako, na kumfundisha yanayohusu maswali haya ya Mithali hii 31. Ni vyema msome pamoja kitabu chote cha Mithali, Mhubiri, na Zaburi. Chukua muda kusoma Neno la Mungu lote kila jioni kwa miaka mitatu, mkisoma sura moja moja na kutafakari na kuwa na maswali mtajifunza mengi ya kulea tabia ya kufaa kwa mtoto. Hakuna kitabu bora kwa kukuza mtoto kama Neno la Mungu.

Je, anaelewa kwamba uumbaji kwa siku sita na mapumziko ni mhimili kwenye mafundisho ya Neno la Mungu? Siku hizi nadharia za kuibuka (evolution)

zimezuka na kufanya mabinti zetu wasijithamini, kwamba wameumbwa na Mungu! Siku za Mwanzo moja ni siku halisi za masaa 24 na si mamilioni ya siku.

Somo la kwanza kwa watoto wetu ni utii. Twarudia "Utii" ndiyo somo la kwanza!". Kutii maagizo ya Mungu na wazazi.

Tunakumbushia tu kwamba maneno haya yalizungumzwa na mama yake Sulemani, akimwambia kijana wake jinsi ya kuona mwanamke bora! Kinyume cha mwanamke bora ni mwanamke wa Mithali 7, ambaye ni 'mwanamke mgeni" (strange woman).

Lazima sisi wanawake tuwe watu wa kusali kwa kukesha na kuwa na mipango/magoli kamili ya kulea, na kuyaweka kwenye karatasi. Kama tunataka tuwe na mabinti wa mithali 31 lazima nasi waone mifano yetu . Hivyo tumwombe Mungu atupe nguvu, tufunge mikanda ili tusaidiane na mabinti zetu. Mabinti wajifunze utii, mipangilio, kujikana nafsi, ustadi, usafi, na kazi.

Wote tungependa tuwe na mabinti waliokomaa kiroho, kiakili, kijamii, , kiuchumi na kimwili pia.

Mwanamke huyu anazungumziwa kwa undani sana. Twaona anatayarisha chakula, anashona nguo zake na za familia, anafanya ujasiliamali, ananunua mashamba na kulima, ananunua nyumba, anapanda mizabibu, anasaidia wenye mahitaji. Ni mwanamke wakupendeka (admired).

Wanaume pia wangependa kuwa na dada, mama, binti au mke kama huyu.. Hata kama mume ni mtu asiyeamini, aweza kubadilika kwa mwanamke kama huyu. Wanawake wana sehemu kubwa katika malezi, twaona Timotheo, mhubiri mkubwa alipata imani toka kwa bibi yake Lois, na kisha mama yake Yunisi. Tusichoke kutenda wema maana tutavuna kwa wakati wake tusipozimia roho.

Wanawake wengine wamekata tamaa kutokana na maisha magumu ya mateso, mwingine alisema "Nimekinywea kikombe." Ni kweli wengine wameangukia pagumu, hata hivyo tusichoke, tusipozimia roho, hata kama binadamu na wale wa familia yetu ya karibu wasitusifu (appreciate) au kutupenda, wito wetu kwa neema za Mungu, ni kuishi maisha ya mwanamke wa Mithali 31.

Mambo haya ni ya kufanya na mabinti zetu wakikua. Pengine yapasa tuwe na vitu vichache ili tuwekeze kwa watoto wetu hazina mbinguni badala ya duniani. Tusifikiri masomo ya shule tu, bali hata nyumbani. Ni vyema kuwa na mpangilio (syllabus) ya kusaidia watoto tabia na taaluma; maana hata hekima ya dunia tunayoikazania sana yaweza kuwa upumbavu kwa Mungu; 1 Kor 3:19. Waweza kuleta topic kwenye maombi, kuhoji watu, kutenda vitu (practical), kujadili, mafungu ya kukariri kutokana na topic, kuuliza maswali, kusoma vitabu vingine vihusuvyo tabia tunazozijadili na mwishowe kutathmini, ili wakue kiroho katika ile nyanja mnayotaka kuijenga.

"Upendeleo hudanganya, na uzuri ni ubatili, bali mwanamke amchaye Bwana ndiye atakayesifiwa. Mke mwema ni nani awezaye kumwona? Maana kima chake chapita kima cha marijani" (rubies); Mithali 31:10. Fungu hili linatuambia

tuombee mabinti zetu kuwa na roho za unyenyekevu, na upole mbele ya Mungu, kuwa tayari kusikia na kulitii Neno lake.

Wape nafasi wamhoji bibi au mama mwenye mvuto wa kumpenda Mungu na kuomba ushauri wake. Wape nafasi mabinti/binti zetu ya kuzungumza na baba, au wajomba zao na kuuliza ni sifa gani iliyowavutia kuoa yule waliyeoa. Je, katika Neno la Bwana wanawake kama hawa ni kina nani? Toa mifano ya hadithi za wanawake kama Debora, Esta, Hulda, Elizabeti, mke wa Ayubu, Ruth, binti za Lutu, Tamari, Safira, Goma, Prisila, Abigaili, Jezebel, Bathsheba, Raheli, na Rebeka.

Soma Tito 2 na andika orodha ya mwanamke amchaye Mungu. Soma 1 Tim 5:3-10 inayofanya mjane athaminiwe na kusaidiwa. Jiulize maswali kuhusu binti yako kama anampenda Mungu, na kama wokovu wake ni muhimu kwake. Je, anapenda kusoma Biblia, au anafurahi akisomewa kama ni mdogo? Je, anaelewa Neno la Mungu? Je, anapenda kumtii Mungu? Je, ana mahusiano na Mungu? Je, akifanya makosa, anajutia dhambi na kuomba msamaha kwa Mungu na wale aliowakosea? Je, anapenda kuwa kama wasichana wa dunia kwa mavazi, michezo na mwelekeo? Je, ana udhaifu fulani wa tabia? Je, anafanya jambo gani kuondokana na udhaifu huo. Je, lile tunda la Roho la Wagalatia 5:22-23 linaonekana katika maisha yake? Je, wawezaje kumsaidia katika nyanja hizi za tunda? Je, anakua akiendana na Mithali 31 na Tito 2? Je, ana magoli ya kumtukuza Mungu na kuwa mhudumu kwa Mungu na familia yake, au anajipenda na kutafuta anasa zake za kuinufaisha tu?

"Moyo wa mume wake humwamini, wala hatakosa kupata mapato," fungu la 11. Mume wake anaona kwamba ni mke anayechukua majukumu yake kwa makini. Lazima tuwatayarishe mabinti zetu kwa hili, kwa kuwafundisha (train). Elimu ya binti yako ni muhimu, na inafanywa nyumbani. Ajue kazi za nyumbani, mpeleke kwa mwanamke ambaye ana bidii ya kufanya majukumu yake vizuri, amhoji kwa nini anafanya shughuli zake kwa uaminifu? Kwa nini awe mwaminifu katika kazi? Jadili naye mifano ya uaminifu kwenye Biblia toka udogoni kama vile Ibrahimu, Yusufu, Daniel, binti mtumwa wa Naamani, Delila, Mikali, mke wa Potifa, mke wa Hamani, Herodias, Hawa, au Tabitha. Umepita wakati wa jando na unyago, mabinti walifundishwa haya, leo hii mfundishe binti wewe na waumini wenzako. Usiseme 'shangazi'vvff ndiyo amfundishe hili.

Mara nyingi wasichana wana majaribu ya kuzungumza mno ubaya wa wengine na kusifia (flattery). Kama wazazi tuepuke kutia chumvi, uongo, umbeya, manung'uniko, wivu, hasira, kiburi na unafiki kwa maneno, matendo na mwelekeo. Mpeleke amhoji mtu kanisani "Kwa nini unamwamini fulani na si Fulani?" Je, waweza kumwamini binti akisema kitu au anasema nusu ukweli na nusu uongo akitoa udhuru? Je, anasema uongo kwa matendo yake na kutunga hadithi, au kupunguza kweli? Je, anatunza ahadi zake? Je, akisema uongo anajaribu kuufunika uongo huo kwa uongo mwingine? Je, anazungumza watu vibaya wasipokuwepo? Je, anarudisha vitu alivyoazima? Je, ana uaminifu katika mahusiano, magoli,

malengo au mipango yake au anajidanganya hata yeyé mwenyewe? Je, anapenda kutoa rushwa au kujipendekeza ili afanyiwe kila anachotaka? Je, anasema kwamba alikuwa 'anatania tu' akikutwa amefanya uovu? Je, mara nyingine anazungumza bila kufikiri na kukosoa wengine bila kujali au kuwa na upole? Je, yupo huru kuja kwako na kukueleza mambo yasipokuwa mazuri na hasa yale nyeti?

Jadili naye maswali kama 'Kwa nini si vizuri mke kumsema vibaya mume, wazazi au hata wenzake kwa watu? Kwanini mwanafunzi hapaswi kumzungumza vibaya mwalimu wake?' Uaminifu ni muhimu utotoni na hata ukubwani. Jadilini ubaya wa talaka na aandike insha.

Je, yupo tayari kumsaidia rafiki endapo amekosea kwa upendo na unyenyekevu, na siyo tu kumsema mbele ya watu na kumwacha aendelee na tabia mbovu? Je, anakasirika haraka na kufuta urafiki kirahisi. Je, anapenda wote wasiwe na urafiki na yule ambaye yeye ameacha kuwa rafiki naye? Je, anasamehe haraka akiwa amekosewa? Je, anathamini mawazo ya marafiki zake au wadogo zake, na kuwasimamia naye pia aweza kuwapa ushauri mzuri?. Je, anakuwa na wivu au chuki rafiki yake au ndugu akifanikiwa? Je, yuko tayari marafiki zake wawe marafiki wa wengine, au anataka wawe marafiki zake tu? Je, anapenda kuwazomea, kuwashushua au kuwabeza wengine akiwa na marafiki zake? Je, anathamini uongozi wa wazazi na magoli ya familia. Je, anakosa adabu kwa wazazi wake mbele ya marafiki zake?. Je, ana uaminifu kwa mume wake wa siku za usoni kwa kujitunza au huingilia urafiki wa kimapenzi na wavulana/wanaume? Je, anajua kwamba ndoa ni jukumu la maisha yote (lifetime commitment)?

Kama msichana, usikivu ni jambo jema, hata kwa mume atakapoolewa. Kuwa msikivu bila kuingilia kati, kubishana au kupayuka payuka liwe lengo lake. Anapaswa kujua mke anamsikiliza mumewe kama kiongozi, akitoa majukumu au kujadili mambo ya familia. Watoto wake pia watahitaji kusikilizwa, hii ni karama anayopaswa kujifunza kuwa nayo. Wanawake wengi twahitaji tusikilize zaidi ya kuzungumza.

Dhambi zinazotuzinga kwa upesi kama vile umbeya, kukosoa, na kutona tona (nagging) zinatokana na kuzungumza sana badala ya kusikiliza. Twapaswa kufundisha mabinti zetu kusikiliza. Kitabu cha Mithali, Mhubiri, Zaburi na barua za Paulo vina mengi kuhusu haya. Angalia watu ambao unafikiri wana hekima, kisha waangalie wakizungumza na watu. Je, wanazungumzaje, wanasikilizaje? Je, wanaulizaje maswali? Je, waweza kujifunza nini toka kwao? Umbeya na kutosikiliza vizuri vina undugu. Je kwa nini ni muhimu mke kumsikiliza mume au mtoto kabla ya kurukia? Mwambie aandike insha ya kumsikiliza mume au mtoto. chukua tangazo la biashara la uongo umpe alitoe kasoro.

Maswali ya kujiuliza kama mzazi ni: Je, anasikiliza sauti ya Mungu na kumtii Roho wa Mungu anapozungumza na moyo wake? Je, anasikiliza mahubiri kwenye nyumba ya ibada? Je, anaweza akarudia yaliyozungumzwa ibadani au anasema mahubiri yalikuwa mazuri, bali hawezi kukumbuka kitu? Je, anakusikiliza wewe

au baba yake mkizungumza naye? Je, anaonyesha adabu ukizungumza naye, Je, anajifanya hakusikia? Je, anapoteza mawazo kwingine watu wakizungumza naye? Je, hana simile ukizungumza naye na anataka aendelee na shughuli zake, na mara nyingine anaondoka ukiendelea kuzungumza? Je, anasikiliza kwa umakini unachomwambia na kukifanya sawa? Je, anakumbuka alichoambiwa? Je, anapenda kuingilia kati mazungumzo na kufikiria atakachosema badala ya kusikiliza? Je, anatoa ushauri wake haraka wakati bado mwenzake anamwambia tatizo lake, Je anapenda kutawala mazungumzo yote?

Kama msichana anatakiwa awe na sifa ya upendo, asiwe mtu wakujifikiria na; na akariri fungu la1 Korintho13: 4-8, na baada ya wiki mbili hivi amalize kukariri yote. Je, akipenda watu ni matendo gani atatenda? Je, akimpenda Mungu na kutaka kufanya mapenzi yake ni matendo gani yataonekana kwake? Je, awezaje kuwaonyesha upendo ndugu zake, baba na mama yake, babu na bibi, Wajomba na shangazi? Je, apaswaje kuwatendea "maadui" zake, kutokana na Neno la Mungu?

Tito mbili yahimiza wanawake wajane wazee kufundisha wanawake vijana kupenda waume zao. Upendo unafundishwa pia, na ni vyema tuwafundishe binti zetu, hasa katika ulimwengu wa leo uliojaa ubinafsi au umimi (me, myself, and I). Wengi wanasema nafanya hili kwa ajili yangu, au "kila mara nawafanyia watu vitu, nimechoka sasa nataka nami nijifanyie!". Wanawake wajane, wanathamini sana waume zao, hasa wakiwakumbuka, wanasema 'ningejua'.

Someni pamoja na kujadili upendo wa aina tatu (Phileo yaani wa ndugu, Agape yaani wa Mungu na Eros yaani wa mapenzi kati ya mume na mke). Je hizi aina za upendo zinatofautianaje?. Je, ana uvumilivu wengine wanapokosea au anapata hasira haraka? Je anaonyesha upendo wa Mungu kwa wengine hata kama haafikiani nao? Je, yupo tayari kusahau makosa madogo madogo ya watu aliyofanyiwa? Je, anapatana na kushirikiana na wengine, na wengine wanapenda awe rafiki yao? Je, anapenda kusaidia mahitaji ya wengine kabla yake au anajitafutia yeye kwanza kabla ya ndugu zake au marafiki? Je, anakimbilia kiti kizuri au andazi kubwa au mwanasesere mzuri ili wengine wasipate? Je, anaangalia mapungufu ya watu na udhaifu wao kupita kiasi? Je, anawakosoa marafiki zake kwenye kadamnasi? Je anapenda kujenga wengine au anapenda kujipigia filimbi yake na kujisifu? Je, anakumbuka makosa ya wengine mara kwa mara? Je, anacheka na kufurahi wengine wakipata adhabu? Je, anatafuta nafasi ya kuhudumia wengine au anataka yeye tu ndiye ahudumiwe? Je, anaonyesha upendo kwa wale wanaotaka kumdhuru au kumwangusha?

Utii na kuwa na adabu ni muhimu sana kwa msichana. Binti zetu tuwatayarishe wamtii Mungu. Ili kuishi maisha ya amani na furaha, ni muhimu kumtii mume endapo Mungu amewapangia kuolewa. Mabishano, kukunja nyuso

saa yote, manung'uniko, kuzira, na kutaka kuburuza wengine si tabia njema. Wote tumeanguka na kupungukiwa na utukufu wa Mungu ila turudi.

Mama yetu Hawa kwa kutotii na kukaa karibu na mume wake, alikuwa mtenda dhambi kwa kwanza duniani. Mara nyingi tunafikiri wanaume wana vituko vingi na dhambi nyingi kama vile kuua, ujambazi, uongo, na mengineyo; bali tukumbuke ni mwanamke ndiye aliyetufikisha hapa kwa kutotii! Mwanamume naye amepewa sehemu yake, ya kumpenda mke wake kama Kristo alivyolipenda kanisa na kulifia. Hii ni kazi kubwa mno pengine kuliko ya mwanamke akiitenda inavyopaswa.

Nilimsikia mama mmoja akisema wanaume wana ukarimu mkubwa kuliko wanawake, na hivyo tunapokuza watoto wa kiume tusisahau hili. Nilishangaa baadaye nikagundua ni kweli kwani mipango yote ya serikali ya kutoa misaada aidha ya ustawi wa jamii au kwa mataifa mengine, wanaume ndiyo wahusika mara nyingi! Hivyo wakina mama, tufundishe mabinti zetu ukarimu na karama tofauti za jinsia na fundisho litafika kwa wajukuu zetu pia! Kwa upande mwingine hasi, wanawake wanagombana na watu hapa na pale au majirani bali wanaume wanaenda vitani na kugombana na wengi! Haya yote mwanamke wa mithali 31 apaswa ajue ili asaidie watoto wake wote. Wanasema Barbra mke wa Bush yule mzee aliyekuwa raisi, alisema haya wakati mtoto wake aliposhika uraisi wa Marekani, nchi yenye nguvu duniani 'nimetawala dunia mara mbili, kwanza mume wangu alikuwa raisi, kisha mtoto wangu wa kiume sasa ni raisi!'. Mama huyu alijua kama mama ana nafasi fulani, si lazima ile mwanamume alipewa, ila ana fungu lake.

Katika kielelezo alichotupa Mungu, si kazi kumtii mume, kwani yaonekana yeye ndiye mwenye jukumu kubwa katika ndoa nasi ni wasaidizi. Kumtii mume ni furaha kubwa na ni amri toka kwa Mungu, na kama huamini, basi mwulize mama mwenye mkamwana (mke wa kijana wake) asiyemheshimu akueleze jinsi serikali hiyo ilivyo na masikitiko yake.

Mtoto wa kike anapaswa kujua agizo la Mungu la waefeso sita "Enyi watoto watiini wazazi wenu katika Bwana maana hii ndiyo haki". Je, ni njia gani binti aweza kuonyesha utii kwa wazazi wake? Je, mamlaka gani mengine zaidi ya wazazi anapaswa kutii? Kanisa, serikali, kazi n.k. Someni Neno la Mungu la wale waliotii na wale wasiotii kama Akani, Kaini, Nuhu, au Yakobo. Soma kumbukumbu la Torati 28.

Je, kwa nini jina la Mungu linaweza kutukwana kwa mtoto asiyemtii mzazi au mke asiyemtii mume? Je, anatii bila kusita, kubishana au kulalamika? Je, anafanya unachomwambia kwa furaha au anaweka sura mbaya? Je, uso wake waonyesha roho ya unyenyekevu mbele ya Mungu na mamlaka Mungu aliyoweka kwa ajili ya maisha yake? Je, matendo yake yanaonyesha utii? Je, anatii mamlaka uliyompa mwingine kama yaya, shangazi au mwalimu? Je, anajua kwamba Mungu Ndiye mamlaka ya mwisho? Je, anathamini maamuzi yako hata kama mara

nyingine hayaleti maana kwake? Je, anajua jinsi ya kukata rufaa kwako kwa adabu endapo anataka asikilizwe tena? Je, anaonyesha adabu kwa polisi, walimu na mamlaka ya serikali? Je, anatumia muda kujua Neno la Mungu na kulitii? Je, anakutii ukiwa karibu au hata mbali ambako humuoni? Je, anatii kwa furaha au kwa moyo mzito?

Kutunza amani nyumbani ni muhimu kwa msichana. Usichana ni maabara ya vile atakavyofanya duniani. Mahusiano mema ni zawadi toka kwa Mungu na kuyatunza na kuyapalilia ni jukumu. Tuwaepushe mabinti zetu na kuzira, kuweka visasi kwa wazazi au ndugu zao. Kuwa na chuki au hila si kitu Chema. Twapaswa tusamehe ili kuleta uponyaji na kukua na hata kukomaa kiroho. Soma kuhusu upatanishi, magomvi, kuonywa, na mwanamke mgomvi kwenye kitabu cha Mithali.

Je adui atendewaje? Mpe binti aandike kuhusu kusamehe wengine na kusamehewa. Soma Neno la Mungu na kuona mifano ya kusamehe na kusamehehwa. Twaweza kujua Neno la Mungu, bali tusipojua kusamehe tutapata maumivu mengi, mahusiano yaliyovunjika na hata kwenda Jehanamu tusipotilia makini. Mahusiano ya binti akiwa mdogo katika familia yanamtayarisha kuwa na mahusiano mema na familia yake atakapokuwa mtu mzima.

Je, wazazi ni watu wa kupatanisha wengine, Je, wanasamehe watu, au wanapenda malumbano? Wewe kama mama angalia pale unapaswa kusahihisha. Jadilini kuhusu mwanamke mgomvi kwenye kitabu cha Mithali. Soma pale wanawake waligombana kwenye Biblia kama vile Sara/Hajiri, Raheli/Lea/Yakobo, Penina/Hana, Mikali/Daudi. Miriamu/Musa, Ayubu/Mkewe uodia/sintike. Waligombania nini? Matokeo yake yalikuwa yapi? Je, tunajifunza nini?

Soma Waebrania 12:15-16 na Jadili na binti. Jadilini kuhusu hasira, visasi, kusamehe na uvumilivu.

Je, anachukuliana vizuri na ndugu zake au kila mara wanagombana akijitetea kwamba anatunza haki yake? Je, ana haraka ya kuzungumza au anasikiliza anapoonywa? Je, anapogombana, anachunguza moyo wake kama ni yeye ana makosa? Je, anasamehe wengine, akijua hata yeye ana makosa pia?

Je, yupo tayari kumfuata aliyemkosea na kumwomba msamaha? Je, anapenda upatanisho au anakaa na kisasi? Je, anajua jinsi ya kutafuta suluhisho kwa njia ambayo haitaleta ugomvi? Je, anasali kwanza kabla ya kuzungumzia upatanisho? Je, yupo tayari kusuluhishwa hata ikibidi zaidi ya mara moja na mtu huyo huyo? Je, anajaribu apatane na waliyekosana mapema au anakaa na hasira muda mrefu? Je, anaamini Mungu atampigania au anapenda kuchukua sheria au kisasi mkono mwake? Je, anaangalia mazuri ya wangine au anaangalia mabaya yao tu? Je, ni mwepesi kukosoa na kukaa na chuki? Je, anasamehe na kusonga mbele au anapenda kuyaleta yale aliyokosewa zamani tena na tena?

Haya ni muhimu kwani binti akiwa na nyumba yake atakosewa na mume au watoto, naye atawakosea pia. Hivyo aanze kujifunza mahusiano ya kutunza amani anapokua.

Lazima ajue unyenyekevu ni jambo muhimu. Kunyenyekea kwa uongozi wa Mungu ili kila siku umimi upungue kusudi Roho wa Mungu aweze kufanya kazi ya kumsaidia kwa tabia njema. Awe tayari kukosolewa bila kubishana. Je, yuko tayari kusema alilokosea bila kuficha? Je, maneno yake yanaonyesha kiburi na anafikiri wakati wote yeye ndiyo yuko sawa? Je, hakati tamaa akifanya dhambi bali yupo tayari kuomba msahama si kwa kuepuka adhabu bali kwa kumpenda Mungu. Je, anajua hawezi akafanya vizuri bila uongozi wa Mungu? Je, anajua kwamba Mungu ndiyo mtawala na amempatia wewe mzazi, umsaidie katika maisha yake? Je, anajua sheria za Mungu ni kwa ajili ya mema kwetu?

Kuishi maisha ya usafi ni muhimu kwa binti, na mji wake atakapokuwa mtu mzima. Usafi wa mawazo, maneno na matendo. Mfundishe kuomba kila siku ili aweze kumtii Mungu na kuepuka majaribu.

Je, majaribu ni nini? Kwa nini tunafanya dhambi, matokeo ya dhambi ni nini? Someni pamoja kwenye Neno kuhusu dhambi na maisha ya giza au mahusiano ya dhambi. Je, wangapi wamefanya dhambi? Mshahara wa dhambi ni nini? Je, ni kina nani walishinda majaribu? Na ni kina nani waliepuka? Someni pamoja Mithali saba na jinsi ya kuepuka tabia ya mwanamke mgeni? Je,anajua kwamba kuna mapambano kati ya Shetani na Mungu na kwamba yeye anahusika? Je, anajua shetani alitoka wapi? Je, anajua akiwa na shida hapaswi kwenda kwa waganga au wachawi bali kwa wacha Mungu? Je, anajua yeye yuko hapa duniani kwa sababu gani?, Je, anajua jinsi atakavyopata ushindi? Je, anajua kulitumua Neno la Mungu kupata ushindi kwa majaribu? Je, anaepuka mahali kwenye mitego ya majaribu au anajipeleka? Je, anachagua marafiki wanaompenda Mungu au wale wanaompeleka kwenye uovu? Je anajua kukimbia majaribu? Je, anakubali mashauri kuhusiana na marafiki wabaya? Je, anakutii katika mambo yote kama vile muda wa kurudi nyumbani au shughuli za za kufanya?

Je, ana tabia ya kutongoza wavulana au kusema vimaneno vyenye walakini vinavyowafanya watu wamshuku mambo maovu? Je, anamwomba Mungu kumsaidia kuepuka dhambi, Je, anaepuka marafiki wa kiume 'boyfriend' na kujua mpango huo wa dating si wa usafi bali ule wa uchumba (courtship)? Je, anatumia muda wake vizuri au anasoma vitabu vichafu au kuangalia picha mbaya? Je anatumia muda wake kuwa na ndoto za mchana zisizo na faida? Je, anakuja kwako kwa maswali ambayo ni nyeti na ya rika yake au anakuogopa (ya uchumba, marafiki wabaya n.k)?

Ni vyema kufundisha mabinti wetu uvumilivu na kuwa na tabia ya mbinguni. Twawafundisha haya wakiwa wadogo kabla ya kupevuka. Wawe na uvumilivu katika mambo mengi, mfano ya kutoanza kuwa na marafiki wa kiume mapema bali kufuata mpango a uchumba. Hatushauri kuanza uchumba mpaka

kupevuka, hii ni  kuanzia miaka 18, ila ni vyema waweze kujitegemea ili wasiwe mzigo. Marafiki wa kawaida (general friends) ndiyo wale ambao mara nyingi ataolewa nao.

Aepuke kuzungumza na wavulana mafichoni, akiwapa matumaini fulani ya urafiki usio mzuri. Ni vyema awe wazi ya yale yanayoendelea kwa vile wazazi wana uzoefu mkubwa, hasa maisha ya leo katika kuwasadiia  mabinti ili wasiingie katika ndoa zenye huzuni. Mama uwe tayari kujadili; mtoto wako hawezi kujifunza kwa mwingine sawa, ila kwako. Ni vyema mama amsaidie binti kuweka viwango vya mume anayetaka kuolea naye, akiwa tayari kutii na kumheshimu mume huyo. Angalia mifano ya Isaka/Rebeka, David/Mikali, Esau, Samson, Solomon, .

Soma vitabu kama, "I Kissed Dating goodbye;" by Joshua Harris na mjadiliane hatari za Dating (urafiki na wavulana) na uzuri wa Courtship (uchumba). Je,yupo tayari kusikiliza mashauri yako kuhusu kuchagua mwenzi wa maisha, Je, anaamimi kwamba Mungu atamsaidia kupata mchumba au anataka kuharakisha? Je, yupo tayari kukua kiroho ili kuwa na nyumba bora au anakimbilia aolewe? Je, anasoma hadithi za mapenzi ambazo zote zina mafundisho mengi ya uongo kuhusu upendo na ndoa?

Je, yupo tayari kujitunza kwa kuepuka majaribu ya ngono yaliyo katika miziki, vitabu, picha, marafiki na filamu? Je, amekuja kwako na kuuliza maswali kuhusu ngono kwa mpango wa Mungu na ngono safi? Je anajua mpango wa Mungu kuhusu ngono? Je, ameelewa kukomaa kwa msichana kwa kuvunja uongo na jinsi ya kujitunza? Chukua muda kuzungumza nayo haya, si mara moja tu, ila hapa na pale. Je, yupo tayari kuishi peke yake maisha yake yote kama ni mwito ambao Mungu amemwitia?

Kujitoa kikamilifu ni muhimu kwa msichana. Twaona maisha ya Ruthu jinsi alivyojitoa kwa mume wake, na kisha kwa familia ya mume wake na kubarikiwa. Binti anapaswa aheshimu wazazi wake akiwa mdogo nyumbani kwao. Awaheshimu ndugu na jamaa kama kaka, dada, mama, baba, babu bibi, mjomba na shangazi. Angaliwe na mfundishe kwa makini, kisha ujiulize haya. Je, anaheshimu wakubwa wake? Je, anawakejeli, au kuwapuuzia wakubwa wake? Je, , anataka bibi na babu wamsaidie yeye bali yeye hataki kuwafanyia kitu? Je,anasikiliza kwa adabu wajomba, baba wadogo, au shangazi zake? Je, anatawaita bibi na babu nakuomba mashauri yao? Je, kwa kawaida anawasiliana na babu na bibi? Hapa wazazi ni lazima tuonyeshe mfano wa kupenda na kuheshimu wazazi wetu. Je, anawasaidia wazee kijijini mwake kwa furaha? Je, anawashukuru ndugu na jamaa wanapomsaidia au anaona ni haki yake?

"Hutafuta sufu za kitani, hufanya kazi yake ya mikono ka moyo" Fungu la13. Twapaswa kuwafunza mabinti zetu kuwa na ujasiliamali au bidii ya kazi. "Asiyefanya kazi na asile." Wanapaswa wafanye kazi, wakijisia au wasipojisikia!  Wajifunze kufanya kazi kwa furaha, kazi ni amri toka kwa Mwenyezi

Mungu kabla hata ya maanguko ya binadamu. Mfanyakazi awepo au asiwepo, binti ajue kufanya kazi zote na azifanye.

Binti afanye kazi za mikono, kazi za shule, lazima tuwe na orodha ya vitu vyakufanya kila siku. Kama ni kulisha kuku, kutandika kitanda, kufua, kufagia, kudeki, kulisha wanyama. Twajifunza toka kwa nyuki, siafu na wanyama wengine kuhusu kutokuwa na uvivu. Chukua muda kuona wadudu hawa na binti. Aangalie unavyofanya kazi, naye afanye akijali wakati atakapojifunza kuzifanya asifanye kivivu. Mpe kazi zingine kwa malipo madogo ambazo si za kila siku kama una uwezo kumpa motisha. Aweza hata kufungua akaunti yake kama familia inaweza kufanya hilo na kujifunza kutunza akiba/kutumia pesa kwa hekima. Someni kuhusu kulala kupita kiasi na hasara zake. Chunguza maisha ya Yusufu, Nehemia, Daniel , Ruth au Tabitha. Angalia maisha ya Raheli na Rebeka wakifanya kazi kabla ya kuchumbiwa. Mkatie sehemu ya bustani ashughulikie. Angalia maisha ya wanariadha, wanasayansi, waandishi, wavumbuzi na masaa waliyotumia. Angalieni wanawake wenye biidii mnaowajua, wanafanya mambo gani? Je, uvivu una shida gani?

Jiulize, Je, anafanya vizuri anavyoweza? Je, anafanya kazi pale watu wanapomwangalia, Je, analalamika na kuweka sura mbaya akitaka apewe zawadi au kulipwa? Je, anangojea mwingine afanye kazi, aking'unung'unika au kutoa vijisababu? Je, anauliza maswali kana kwamba hajui kufanya kazi uliyompa, au inakuwa sababu kwake ya uvivu? Je, anafanya kazi za kila siku bila kukumbushwa? Je, anamaliza kazi au anapotea au kupeleka mawazo pengine? Je, waweza kumweleza jinsi kazi inavyofanywa na akaifanya? Je, anafanya kazi nusu nusu? Je, anatunza vitu vyake? Je, anarudisha vitu vyake baada ya kutuvimia? Je, anacheki kazi yake kabla ya kuripoti au anaparaza paraza tu? anapoteza muda, au kusema nitafanya kesho? Je, anakata tamaa na kuacha kufanya kazi inapokuwa ngumu?

"Afanana na merikebu za biashara, huleta chakula chake kutoka mbali, tena huamka kabla haujaisha usiku;" fungu la 14. Tabia ya uzalishaji mali, bidii ya kazi na utunzaji wa mali ni muhimu sana. Mtoto wa kike afundishwe bidii ya kazi za mikono, jinsi ya kutunza pesa, jinsi ya kufanya bajeti, jinsi ya kununua vitu sokoni au dukani. Kama kuna uwezekano alinganishe bei kadhaa au masoko tofauti kabala ya kununua. Afunzwe ubaya wa ubaradhifu au utumiaji mbaya wa vitu kwa kufuja. Ajue jinsi ya kununua chakula chenye lishe bali chenye bei nafuu. Afundishwe uchuuzi, kuona thamani ya kitu na kuweza kuzungumza apunguziwe kama inawezekana (bargain). Je, akinunua vitu kwa jumla, au vingi bei inakuwa ndogo au kubwa? Je, akipika chakula kingi akigawe mara mbili kwa kutumia siku moja, inasaidia matumizi ya pesa?

Mfundishe jinsi ya kununua , afanyeje ili aweze kuweka akiba? Afundishwe kufanya bustani ili kupunguza makali ya kununua kila kitu, hasa mboga. Je, anajua kutafuta nguo za mitumba zilizo nzuri na za kuzimachisa vizuri zipendeze, aidha

kwake au kwa wadogo zake? Familia nyingi zinaingia gharama kwa burudani (recreation) ambazo ni ghali, je anajua burudani za kufaa na zisizo na gharama?

Niliona pale Dar es Salaam familia za wahindi wanaenda baharini kupunga upepo, na kula chips za mihogo au madafu kwa bei nzuri. Wakati familia nyingine zinaenda kwenye burudani ambazo ni ghali mno wakila kuku wa kukaanga kwenye hoteli kubwa soda, pizza, icecream na vyakula vingine Ghali, na ambavyo siyo vya afya. Haya yote ni muhimu kuwafundisha watoto wetu.

Je, chakula kinachobakia anaweza kukitunza na kukitengeneza vizuri kifae? Mabaki ya mboga, na maharage machache, aweza kutengeneza supu na kuongeza vitu vingine. Je, wageni wakitokezea ghafla anajua jinsi ya kuongeza chakula kidogo kitoshe wengi? Afundishwe kufuga kuku wa mayai au ng'ombe wa maziwa kama kuna uwezekano. Msichana afundishwe kutunza chakula kwa wakati wa kiangazi.

Zamani makabila mengi yalikausha mboga za majani, viazi vitamu n.k. siku hizi hatufahamu haya. Wakati wa mvua tuna mboga nyingi, ila wakati wa kiangazi tunapata shida. Angalia kama ananunua visivyohitajika bila kufikiri. Je, anakubali matangazo ya biashara ya kununua vitu kirahisi? Je, yupo tayari kununua vitu ambavyo vimeshuka bei, au ana uvumilivu wa kungoja? Je, anajifunza kushona, kufuma na ustadi mwingine kupunguza matumizi? Je, ukimtuma sokoni, anaweza kulinganisha bei na kuleta vitu vya nafuu na vizuri. Je ukimwandikia orodha ya vitu vya kununua dukani, anavifuata, au ananunua usivyomtuma? Je, akiingia sokoni anajua tofauti kati ya vyakula vya lishe bora na vyakula visivyo na lishe (junk food)? Je, anaweza kufuata bajeti na kuitumia? Je, anaacha acha vitu vyake bila kujali viharibike?

Msichana afundishwe jinsi ya kutumia muda vizuri. Muda ni talanta ya ajabu, ambayo kila mtu amepewa. Mtoto afundishwe jinsi ya kumudu muda na kukomboa wakati ili aweze kumsaidia mume wake, watoto, jumuiya na kanisa. Mfundishe jinsi ya kupanga muda katika kufanya kazi za nyumbani. Mpe mradi wenye muda wa kumaliza (deadline). Tengeneza naye list ya mambo ambayo mnayoweza kumaliza kwa dakika tano, kumi na kumi na tano. Talanta ya muda ina thamani kubwa.

Atembee na kitabu anapokuwa anangojea basi, afume au afanye jambo fulani. Vitabu vya kumsaidia kimaisha (long life learning). Angalia jinsi muda ulivyoikuwa muhimu katika uumbaji kwenye Mwanzo moja. Tengezeni ratiba ya kutumia kwa siku nzima, mfano kuamka, kupiga mswaki na kuoga, kusoma Neno la Mungu. Mpatie muda awahoji watu wazima kwamba wangerudi nyumba ujanani ni nini wangefanya tofauti.

Je, majuto gani ya kupoteza muda au kutofanya jambo? Je, ni short cut gani zatakiwa ukipika, ukisafisha nyumba au ukishona? Je, ni jinsi gani mtu abajeti muda wake? Je, wafuatao walitumiaje mida yao kwa hekima? Daudi, Josiah? Kristo? Daniel, Miriam, Yusufu, Musa, Samueli. List shughuli ambazo zinafanyika

kwa kipindi fulani tu katika maisha ya msichana mfano elimu, kuzaa watoto, ndoa, uzeeni. Mwulize kama anafanya yanayotakiwa kwa wakati wake.

Nunua daftari la kupanga muda na kalenda ya mwezi mirejee kila wiki. Jiulize kama anatumia muda wake vizuri kupanga maisha ya baadaye au ni kucheza na kupoteza muda. Je, anatumia muda kuwekeza kwenye umilele kwa kusoma Neno la Mungu na kuomba. Je, ana ratiba ya kila siku au anakaa na kuwaza ndoto za mchana. Je, muda wake wa mapumziko anatumia vizuri? Je, apoteza muda kwenye simu, tv na computer? Je, akipewa kazi anapoteza muda au anatunza muda? Je, anachukua muda mwingi kujirembesha? Je, analala, ana ratiba anayoifuata. Je, anawahi kanisani na shuleni au appointment nyingine? Je, anapenda kusema nitafanya kesho au kungoja kufanya mambo dakika ya mwisho? Je, anaweza kufanya shughuli mbili au tatu kwa wakati mmoja au akingojea maharage yaive, anakaa hapo hapo kisha ndiyo anainjika mboga? Je, angaalia njia za faida za kutumia muda wake kwa hekima?

Kama msichana na baadaye mama mwenye kushugulikia mume na watoto, ni vyema ajue kufua nguo, kujitunza kwa usafi katika mambo yote ya kike, kupika, kukomaa na shughuli zote za nyumbani. Je, anaweza kugawa majukumu kwa wadogo zake, na hatimaye hata akiwa na msaidizi wa kazi aweza kumwambia cha kufanya bila kupoteza muda? Aangalie jinsi ufanyavyo kazi na kuzigawa kwa wengine wakusaidie. Angalia vifaa ambavyo unafanyia kazi na mwelimishe, naye aanze kununua pole pole anapopata visenti. Vifaa hivi ni kama cherehani, sindano, jembe, masufuria n.k.

Je, anajua kutumia cherehani, na hata kukarabati nguo zake? Je, anajua kutumia sindano, kukarabati nguo, kushona vifungo, au kufuma vitambaa. Je, anaweza kusoma pattern ya sweta, kitambaa cha kufuma, au nguo ya kushona?

Chukua pamoja na binti yako project fulani mfano kupamba ukumbi wa harusi na andikeni jinsi mtakavyofanya shughuli hatua kwa hatua na kuimaliza.

Angalia maisha ya Yusufu, Debora na Daniel. Je, Mungu aliwatayarishaje ili waweze kuwa watawala? Mungu anatayarisha wasichana wetu kuchukua majukumu ya kutunza familia zao na mengineyo. Angalia kama anamaliza shughuli unazompa. Je, aweza kuivunja project kubwa kwenye kazi ndogo ndogo na kuwapa wengine wamsaidie? (delegation), Je, anafundisha wadogo zake kwa uvumilivu?, Je, anapopewa kazi ya kusaidiana na wengine, anataka aifanye yeye mwenyewe? Je, anaweza kuelewa maelekezo ukimpa (directions). Je, aweza kukagua kazi ya wengine ambao wako chini yake? Je, anaongoza wengine kwa unyenyekevu au anawakandamiza na kuonyesha kwamba yeye ndiye bosi? Je, anasaidiana na wadogo zake kufanya kazi au anawatazama tu? Je, wengine wanapenda kufanya kazi naye au wanamuepa?

Mwanamke anaweza kupika milo 1000 kwa mwaka, wengi wanakumbuka vyakula vya mama zao. Ni muhimu tuwafundishe watoto wetu kupika vizuri. Tujifunze hata na mapishi mengine ya makabila tofauti na kupanga

vya kupika, kutoka kwa vile tunavyolima na vile ambavyo ni rahisi kwa msimu ule. Je, anajua kiasi gani kila mtu katika familia anapaswa kula? Siku hizi za utandawazi aweza kupata mapishi toka sehemu mbali mbali kama vitabu, tovuti na mengineyo. Je, mwaweza na yeye mwandike kitabu chenu cha mapishi rahisi cha kutumia na kanisa lenu?

Wataalam wanasema kwamba mapishi yoyote yakiwa na zaidi ya vitu saba si mema kwa afya. Mfundishe kupika,si kwa vikolezo vingi ila kwa afya, kisha ladha na baadaye mwonekano. Kuna mapishi yayonachukua muda mfupi kupika, mengine yanachukua pesa chache. Ulizia marafiki, makanisani na ndugu mapishi mapya, na yakusanye muyaandike. Mwaweza kujitolea kanisa lenu kuwa na darasa la upishi kila mwezi mara moja kwa masaa matatu hivi.

Je,vifaa gani vyahitajika kwa pishi. Je, mwaweza kujifunza kupika mikate, kutengeneza jam au peanut butter? Angalieni magazeti ya upishi. Hoji wakina mama "Kwa nini wakati wa kula ni muhimu?" Je, anajua kuoka? Kukaanga? Kuchemsha? Je, anaweza kutumia vifaa vya jikoni kwa ustadi, usalama, na kuvitunza vizuri? Je, anaweza kufuata maelekezo ya mapishi (recipe) fulani? Je, anaweza kupikia watu wakiongezeka mara mbili? (Mfano ugali wa watu sita badala ya watatu). Je, aweza kupika kwa wakati na kutenga chakula mezani? Je, anajuaje chakula kimeiva? Je, anasafisha vyombo alivyotumia baada ya mapishi?

Je, mama akiumwa anaweza kumudu mambo yote mwenyewe? Je, anaweza kutengeneza chakula kitamu na cha kupendeza? Je, wale anaowapikia ni muhimu kuliko chakula anachotengeneza? Je, anapenda vyakula ghali vya mapambo mengi badala ya kubana matumizi na kupika vyakula vyenye lishe? Je, anaweza kubajeti chakula cha mwezi. Je, anakusanya mapishi mazuri na kujifunza yale yanayowezekana? Je, anajua kuwapikia watu wenye shida maalumu za afya kama kisukari, allergy, moyo au presha? Je, anapenda kuendeleza talanta ya kupika na kuuza chakula? Kama mama je, upo tayari kumsaidia muanze genge dogo (restaurant)? Je, mambo gani ni muhimu yahusuyo chakula mbali na kwamba kina lishe nzuri na kina ladha tamu?

Mambo mengine ya kuangalia ni kupangilia mambo. Fungu la 15. Kupanga nyumba vizuri, kunaleta mawazo kutulia, na pia kunaakisi tabia ya Mungu ambaye ni wa mipango na uzuri (beauty). Tunaowaalika wanapenda waje zaidi kama nyumba zetu zina utulivu na mipangilio. Binti aliyejifunza kupanga vitu akiwa mdogo atakuwa msaada kwenye familia yake na hata atakapofanyia kazi.

Watu wengine wanazaliwa na talanta ya kupanga vitu vizuri, kama wanawake wa mashariki ya mbali, wanapangilia maua vizuri bila kutoka jasho sana; ila wengi wetu tunahitaji kufundishwa na kuhimizwa tena na tena. Kama wewe mama si mpangiliaji mzuri wa mambo, kama mimi, tafuta msaada kwa kusoma na kwa wengine.

Sheria ya kwanza mbinguni ni mpangilio (order). 1Kor:14:40 yasema kila kitu kifanyike kwa mipango. Mabinti wadogo wakicheza warudishe vitu vyao.

Wajifunze kutandika vitanda vyao. Asubuhi mpange siku yenu na hata kuandika, mnavyotaka kufanya, la sivyo siku itaisha bila kufanya mengine. Jifunzeni jinsi ya kupangilia mipango yenu kwenye kalenda, au daftari. Wafundishe watoto kupanga vitabu vyao, picha, wanasesere, meza za kusomea, barua, kazi za shuleni, n.k. Wafundishe kupanga magoli, ya muda mrefu na mfupi.

Panga nao jiko, makabati yao, makabati ya vitabu. Pangeni pamoja na kuwafundisha jinsi ya kutoa kipaumbele (priority) katika mipango. Mkitaka kwenda mahali, kama safari pangeni pamoja, vitu vya kuchukua, ramani, kubook hoteli, simu zinazohitajika, tarehe za kwenda, mahali pa kupita, na vitu vya kufanya. Panga na mtoto ratiba ya siku ya kukaribisha wageni au karamu ndogo. Wekeni bajeti na jinsi ya kuifuata. Pangeni michezo, mapambo, na jinsi ya kupata pesa za kufanya hii karamu. Mkiweza someni vitabu vya Don Aslets "Clutter's Last Stand" au "Clutter free".

Tembeleeni nyumba za wanawake waliopanga vitu vizuri na kwa idhini yao tazameni jinsi wanavyopanga jiko, makabati, au sebule. Pangeni pamoja rekodi za nyumbani za afya, kama chanjo, huduma ya kwanza, na mihadi (appointments) ya kumwona daktari. Pia vyeti, kama vya kuzaliwa (birth certificate), ripoti zao za shule, viweke mahali maalum.

Chukueni faili jipya na kugawanya sehemu na kuandika namba za simu na address za watu, appointment za kalenda kama michezo/matukio, maelekezo kwa yaya, size za nguo za watoto wa nyumbani. Kila moja kwenye ukurasa wake. Weka hichi kitabu mahali mnapoweza kukipata na kukirejea (refer). Angalieni mahali nyumbani ambapo hapa mipangilio na kufanya pamoja baada ya kupanga la kufanya.

Mpe binti kazi ya kuweka picha vizuri na kuzilabel kwenye photo album. Pangeni pamoja risiti, marakaratasi ya bima au picha za kufundishia kanisani. saidiana na binti kupanga chumba chake na kukipamba kwa bei isiyokuwa kubwa. Soma www.Titus2.com wameandika kuhusu kumudu nyumba (managers of their home). Mwambie binti aandike insha ya "Thamani ya nyumba yenye mpangilio."

Je, anaweka kila kitu kinapotakiwa, hata akivua nguo zake usiku haziachi kwenye sakafu? Je, anarundika vitu badala ya kupanga. Je kabati, pochi, begi la shule, lina mpangilio? Je, aweza kupanga mizigo yake vyema akienda likizo toka shuleni. Je, anavitupa tupa popote? Je, ana shida kupata vitu anapotafuta kama vile sindano, uzi, kazi ya shule au viatu vyake? Je, aweza kupanga mahali palipovurugika? Je, anaweza kutoa kipaumbele kipi aanze kufanya? Je, anapenda kukusanya vitu hata visivyo vya maana "junk" na hataki kuviachia? Je, anaweza kutunza mihadi (appointments), anuani, na namba za simu bila kupoteza? Je, ni mtu wa mipangilio sana kichwani kiasi kwamba anapata hasira mipango ikibadilika? Je, unaweza ukamwachia nyumba ukaenda kwa siku moja? Je, anaandika mipango yake ya muda mrefu?

"Huangalia shamba, akalinunua, kwa mapato ya mikono yake hupada mizabibu;" fungu la 16. Fungu hili laonyesha mipangilio ya kununua vitu, kupangilia kutunza mbegu na kupanga jinsi shamba litakavyokuwa kwa mfumbo wa ufanisi na mazao bora. Hata kama ni mdogo, aweza kazi ndogo, kama -kuosha vyombo, kufua, kusafisha nyumba, kutunza wadogo zake, kwenda sokoni, kubadilisha nepi watoto. Kufanya kazi kutamsaidia kupanga mambo makubwa.

Wengi wanakazania shule, na hilo ni zuri, ila watoto wanasoma ili wapate kazi hatimaye. Kila anachofanya kina maana kwa Mfalme wa mbinguni kupata utukufu, na pia kinajenga tabia ambayo ndiyo pekee atakwenda nayo mbinguni.Tusidharau mianzo midogo, ndiyo inajenga watoto wetu kuwa mwanamke hodari na shujaa. Aanze kuweka magoli ya vikazi vya kufanya kabla ya kucheza. Mkatie kazi ndogo ndogo afanya na upange naye kadiri anavyozidi kukua.

Aweza kuanza kupanga magoli ya vitu vya kufanya vidogo vidogo hata vya ujasiliamali kama amefika miaka zaidi ya 14 hivi. Je, ana magoli gani ya kiroho siku za usoni kama kuonyesha upendo wa Mungu? Magoli ya mwanamke lazima yaendane na mume wake, jadilini kwa nini? Je, kuna kitu ambacho ni kigumu ambacho Mungu anataka ufanye katika maisha yako? Je, anapenda kumpendeza Mungu na kumpa utukufu na hilo ndiyo lengo lake kuangalia ya milele badala ya ya muda? Je, malengo yake ya baadaye yanaendana na maandiko ya Mungu au ni ya anasa? Je, ana mipango ya anayotaka kufanya kila siku, na magoli ya baadaye, na anayaandika? Je,anaafikiana na malengo yenu ya familia na kuwaunga mkono kihali na mali? Je, yupo tayari kukosa raha za muda akilenga magoli yake? (mfano kusomea mitihani, badala ya kucheza). Je, ana shauku ya kujifunza mambo mapya, na kutumia ustani huu? Je, anajua Yesu anakuja na ni muhimu kujitayarisha kwa tukio hilo kubwa kupita yote?

Twaona bustani inasaida mambo mengi katika maisha ya mwanamke. Kwa kawaida inabariki anayelima na wengine pia. Bustani inaweza ikaleta uzuri, mazoezi, na hata mahali pa mtu kupumzika na kubarizi. Bustani si lazima iwe kubwa, nimeona wengi marafiki wa mjini wameweza kuweka maua au nyanya kwenye makopo, wakala mpaka wakagawa. Furaha ya kupanda mbegu na kuona zinakua ni muhimu. Kila msichana ajifunze kupanda mboga, na maua pia! Apate mafunzo ya kulima bustani kwa ufanisi, maana ni huduma nzuri kwa wale wenye mahitaji.

Wengi tulio na bustani tumetoa mazao kwa watu ambao ni wahitaji, na kubarikiwa. Ni vyema binti aandike insha ya faida za kuwa na bustani. Je, anajua tofauti ya magugu na mimea? Ukiwa unafanya kazi bustanini unafanya naye? Je, anajua kutayarisha udongo kwa ajli ya kupanda na jinsi na mahali pa kupata maarifa ya kilimo? Je, anajua jinsi ya kukabiliana na wadudu waharibuo mazao? Je ,anauliza ushauri kwa watu wengine maarifa ya kilimo? Je umempa kipande

chake cha bustani alime? Je, anaweza kupangilia jinsi ya kuendesha bustani, na kufanya hivyo kwa msimu mmoja?

Mwanamke huyu wa mithali anapofanya mipango ya kununua na kulima, anakuwa ni mjasiliamali na mwenye kujua jinsi ya kupanga matumizi ya pesa vyema. Kwa vile mabinti zetu watakuwa wakubwa na kuwa na majukumu ya kutunza pesa zao, za waume zao na kusaidia watoto katika mipango mbali mbali; kumfundisha mipangilio ya fedha ni muhimu (financial training). Mtoto afundishwe kugawa pesa zake apewapo, kutoa fungu la kumi, na kuliweka kwenye bahasha au mahali tofauti. Kisha fungu la akiba, na fungu la matumizi. Ni vyema kusoma visa vya Marko 12: Mjane wa senti mbili; Mathayo 25 kwa mafundisho ya talanta na Luka 12 kuhusu tajiri aliyekuwa na mali nyingi.

Binti aulize watu mbali mbali, na hata wazazi kumsimulia mibaraka ya Mungu kwa wale waliorudisha zaka. Masomo ya tamaa ya pesa, kutumainia utajiri, kukopa na ubaradhifu wa pesa, ni muhimu. Mtoto afundishwe magoli ya fedha ya muda mfupi na muda mrefu. Je, atapataje pesa ya kununua kitu anachotaka? Wazazi wajadili, na kama kuna njia ya kumsaidia kufanya biashara ndogo ndogo, basi ni vyema kufanya hivi. Mtoto afundishwe kwamba kutoa ni bora kuliko kupokea, na Mungu hutubariki tunapotoa bila kunung'unika. Panapo nafasi mtoto afunguliwe akaunti.

Je, ni kanuni gani zitumike tunapokopa vitu? Je, aweza kulinganisha bei za vitu kabla ya kununua?Angalieni mifano ya Ibrahimu, Ayubu, Sulemani, Zakayo, Safira na Hezekia. Wekeni kumbukumbuku ya matumizi pamoja kwa mwezi. Fanyeni bajeti ya nguo kwa mwaka. Angalieni kanuni njema za kumkopesha mtu pesa. Awahoji wanawake wachache jinsi wanavyotunza pesa au kuweka akiba.

Je, kuna tofauti gani kati ya sadaka na zaka? Je, anatoa zaka na sadaka kwa ucheshi? Je, mke anawezaje kumsaidia mume wake kwa kuwa wakili mwema wa mali? Unapofanya bajeti ya nyumbani mshirikishe aone matumizi ya nyumbani ya kila mwezi. Ni yapi tunayotumia pesa kila mara tunayoweza kuyakata au kupunguza? Je, kuna uzuri gani wa mke kukaa nyumbani au kuwa na kibarua nje ya nyumbani? Je, anajua kwamba yote aliyo nayo amepewa na Baba wa mbinguni? Je, ana shukurani kwa Mungu aliyempa?

Je, anajua kuweka akiba au anatumia pesa bila kufikiri? Je, ni bahili au yupo tayari kukirimia wengine kwa vile alivyobarikiwa na Mungu? Je, anatumia pesa kwa fujo? Je, anapenda kukopa kopa, au kutumia zaidi ya alivyo navyo? Je, anapenda kutumia pesa kwa anasa za muda badala ya kutunza? Je, anaweza kubajeti kutokana na pesa alizo nazo?

"Hujifunga nguvu viunoni kama mshipi; hutia mikono yake kwa nguvu;" Fungu la `17. Kama vile mwanajeshi aendavyo vitani kwenye Waefeso 6:17, anavyokuwa, ndivyo tunavyotakiwa na mabinti zetu. Ili mabinti zetu waelewe neno vizuri twapasa kujifunza nao kwa mfumo na mpangilio ili waelewe mafundisho makuu ya imani (doctrines).

Kila mtoto awe na biblia yake na akifika miaka saba hivi apaswa kuwa na muda wake wa kusoma Biblia, japo kwa dakika kumi. Pengine itakuwa vyema apate Biblia yenye lugha rahisi kwa kuanzia. Tumekuwa tukitumia Clear word Bible au International Children Bible.. Ila hatuna Biblia za watoto za Kiswahili. Kwa sasa tumeanza kuandika Biblia ya watoto au hadithi za Biblia za watoto, tuombeeni ili tuweze kumaliza kazi hii.

Hatuwezi kumjua au kumpenda Mungu bila kusoma Neno lake. Na Uzima wa Milele ni kumjua Mungu, kumtegemea, kumtumiani na kutembea naye siku kwa siku; Yohana 17:3. Kuomba ni sisi tunazungumza na Mungu na kusoma Neno la Mungu, ni Mungu anazungumza na sisi.

Mama kama mzazi, lazima awe mfano. Je, watoto wanakuona unasoma Neno la Mungu kila siku? Mtoto aanze kuvikariri vitabu vya biblia 66 kwa mpangilio, au pengine kwa kutumia wimbo. Anakili vipande vya Neno la Mungu na kukariri. Kila siku mwaweza kusoma Mithali moja. Kusoma Neno la Mungu ni kitu cha kila siku, kama tunavyokula. Endapo tunaona tu busy sana, dawa ni kutokula chakula mpaka tumesoma Neno la Mungu. Tutajikuta tunasikia njaa na tutasoma. Mtoto anapojua kusoma tu, aanze kusoma Neno la Mungu. Muwe na chati ya kusoma kila siku, pengine kurasa moja, kwa siku au sura moja kwa siku.

Someni historia jinsi Neno la Mungu lilivyotufikia na mambo machache ya Biblia; mfano lugha iliyotumika, vitabu vya torati, historia, mashairi, zaburi. ilichapishwa mara ya kwanza 1456 na mashine ya Gutenberg, imebadilisha maisha ya wengi, iliandikiwa kwa miaka 1700 na watu kama 40. ina sura 1189 si kitabu cha mashauri bora au mawazo mazuri tu bali ni sauti ya Mungu na mamlaka ya mwisho duniani na mbinguni!

Binti asome Biblia na kuweka jina lake mfano 1 Kor 13. Pale penye Neno upendo aweke kwanza jina la Mungu kisha asome mara ya pili na kuweka jina lake. Kariri ujumbe (theme) muhimu katika kila kitabu cha Biblia. Mpeleke binti ahudhurie masomo ya Biblia kanisani (Bible study). Someni pamoja Zaburi 119 na jadilini. Angalieni njia mbali mbali za kusoma Biblia na kuomba neema ya kutenda yaliyoandikwa. Mwandikishe binti kwenye masomo ya Biblia ya Posta au ya online, kama amazingdiscovery.org, na amazingfacts.org, secretunsealed au voiceofprophecy bible study. Akisoma fungu ni vyema aandike yafuatayo: Fungu hili linasema nini? Je, lina maana gani? Linawezaje kutumika maishani mwangu? Je, nifanyeje na hili fungu? Baada ya wiki aangalie kama kuna kilichobadilika kwa katika maisha yake kwa sababu ya lile fungu.

Je, anasoma Neno la Mungu kila siku bila kukumbushwa? Je, ana shauku ya kulisoma? Je, linabadilisha maisha yake na kuleta maana? Je, anaweza kutoa mifano, pale Neno la Mungu linaweza kutumika katika maisha yake? (application). Je, anauliza maswali akilisoma? Je, anashare na wengine? Je, anatafuta majibu kwa maswali yake kwenye Biblia? Je, anaweza akapata fungu kirahisi? Je, anajua

angalau kwa mbali historia ya Biblia? Je, anajua jinsi ya kutumia mbinu za kusomea biblia kama kamusi, na marejeo mengine

Ni vyema mno kukariri Neno. Katika majaribu utamshinda mwovu kwa ahadi unazokumbuka tu! "Imeandikwa". Neno la Mungu tukiliweka moyoni kwetu ndiyo silaha kubwa ya kutotenda uovu; Zaburi 119:10. Roho wa Mungu atatukumbusha pahali pa kutoa upanga kwa jaribu Fulani. Aanze kukariri fungu moja kila wiki. Watoto wadogo wana kumbukumbu nzuri, na kwa vile hawana mengi kichwani, itasaidia. Hakuna jambo linaloleta akili kupanuka na kuwa na wingi wa maarifa kama kukariri Neno la Mungu. Jadilini anapoendelea kukariri ili aelewe maana ya mafungu haya. sura za kuanzia kukariri ni kama Zaburi 23, au 91. 1Kor 13; Amri kumi za Mungu au hata kitabu cha waefeso cha mahusiano, ni kizuri sana. Waweza kurekodi vile alivyokariri. Ni vyema kuwa na daftari la kuandika yale mnayosoma. Je, anaweza kukariri mafungu 20?

Kumfundisha binti mazoea ya kuomba kila siku ni muhimu, kwa vile hata atakapokuwa mtu mzima atajua kumletea Mungu shida zake, na katika shida atakazokuwa na familia yake itamsaidia kutatua matatizo kwa maombi. Daima tufundishe wote tunaowashauri kumpa Mungu shida zao. Ombeni pamoja asubuhi na jioni, aombe mwenyewe pia. Jadilini pamoja sala kuu ya Bwana katika Mathayo sita. Kila mara anapojaribiwa kumzungumzia mtu vibaya, aombe. Awe na daftari dogo la kuandika anayoombea na tarehe. Itamsaidia kurudi na kumshukuru Mungu. Aombee wenye shida, serikali, familia, shule, wazee, kanisa, waliokata tamaa, wagonjwa. Ajifunze kuombea wanaomuudhi. Kumsifu Mungu, kuungama dhambi, kumshukuru Mungu na kuleta haja zenu iwe sehemu ya kila ombi.

Awahoji watu wa imani, wamishonari au wahubiri jinsi maombi yalivyofungua njia, au jinsi Mungu alivyojibu maombi yao. Je, wanawake gani walienda kwa Kristo kumwomba jambo fulani? Andikeni ahadi za Mungu na jinsi ya kuziomba? (zipo zaidi ya 3500). Aanze kuombea mume atakayemwoa japo ana miaka kumi na, tu.

Asome visa vya imani kama cha Hana, Musa, Sulemani, Nehemia au Daudi. Someni maisha ya Agustine, John Newton na wengine wanaoshukuru maombi ya mama Zao yaliyoleta tofauti katika maisha yao. Jifunzeni kanuni za maombi ya kufunga jinsi binti anavyokua. Je, anafumba macho akiomba? Je, maombi ni kitu halisi kwake, yaani mawasiliano halisi na Mungu au ni mapokeo tu? Je, anaomba uongozi wa Mungu kabla ya kufanya maamuzi? Je, anafikiri kuomba akiwa na shida? Je, anaonyesha kicho kwenye maombi, au anazungumza na kuchezacheza? Je, anaamini Mungu anajibu maombi? Je, unamwambia maombi yako yaliyojibiwa kupitia kwake? Je, anatoa shukurani kwenye maombi yake, au anaomba vitu wakati wote?

Ni vyema kuwafundisha mabinti zetu kutawala nafsi. Kukabili miili yao au hisia zao. Ni muhimu sana kujikana nafasi, kwenda kulala kwa wakati na kuamka kwa wakati. Kusoma Neno na kuomba mara baada ya kuamka. Kula kwa

wakati na kujifunza kanuni nzuri za kutunza mwili (kupiga mswaki, kuchana nywele, kukata kucha, kuoga, kufua nguo) bila kukumbushwa.

Ajifunze kula akiwa na njaa, si kwa sababu hana kitu cha kufanya hivyo chakula kinakuwa rafiki. Asile mlo mpaka masaa manne au matano yapite. Uvivu, ulafi, kuvaa nguo zisizo na heshima, maisha ya uovu, marafiki wabaya ni mambo ya kuyakana.

Je, anasikiliza muziki wa aina gani? Aulize wengine wamwambie vitabia alivyo navyo ambavyo vinawachukiza wengine ili aviache kwa neema ya Mungu. Je, anajua chakula cha afya na kufanya mazoezi, au anakula chochote bora anakifurahia? Je, anajua Neno la Mungu lataka tuleje?

Asome maisha ya watu waliojikana nafsi ili kufanya mambo makuu katika maisha, mfano Daniel, Esta, Yusufu. Aandike insha ya 'Ulafi'.

Mkae mahali barabarani watu wanapopita muangalie watu. Je, wanavyotembea, macho yao, nguo zao au mtembeo wao unaleta mawasiliano fulani? Je, yupi atakuwa anajiamini, anajikana nafsi, au mvivu? Neno la Mungu linaitaje miili yetu? Soma hasara za kula mno au kula kidogo? Soma hasara za kula chakula kisicho na afya (junk food) au kile Mungu anasema tusile.

Kuna dhambi zinaathiri miili yetu kama vile hasira na zinginezo, zichambueni hizi. Soma sheria za afya na ulaji kwenye agano la kale kama toka wakati wa Nuhu kabla ya wayahudi. Angalia kama anajitahidi kuishi maisha ya afya,na usafi bila kukumbushwa, anapiga mswaki? Anafua nguo zake za ndani kila siku? Anaoga kila siku bila kukumbushwa? Je, anafanya mazoezi, na kujikana nafsi katika ulaji wake? Je, anajua kwamba mwili wake ni hekalu la Roho Mtakatifu?

Je, mwonekano wake unaonyesha kujikana nafsi na kujiheshimu? Je, anatawala mwili wake ili asiwakere wengine? Je mara zote anaonekana amechoka? Je, mara nyingi ni mgonjwa? Je, anakaa kwa adabu? Je, kuna mambo ya kumsaidia ili awe na afya na nguvu? Je, anatabia za wasiwasi (nervous) kama vile kula kucha zake? Je, anajali anavyoonekana kwa watu? Je, anajali kupita kiasi mwonekano wake kwa watu?

Ni muhimu kuwafundisha mabinti zetu kupata ushauri unaofaa. Mungu ndiye mshauri mkubwa, ila ameweka watu pia watusaidie. Aweza kuwauliza wanawake watu wazima wacha Mungu. Atakapokuwa mtu mzima mara kadhaa atahitaji mashauri ya watu. Ni vyema kuwa wanyenyekevu kuuliza ushauri kuliko kuharibu mambo pale tunapokwama. Neno la Mungu katika Yakobo moja, lasema yoyote kati yetu asiye na hekima aulize, na Mungu atampa. Awaulize wazazi mahali ambapo katika maisha yenu mmeomba ushauri na kufanikiwa.

Kitabu cha Mithali ni kizuri kukisoma na kila mara asema "Mwanangu sikiliza mausia yangu….". Je, atafutaje mshauri bora wa mambo ya kiroho, mambo ya nyumba, mambo ya jamii au mambo ya fedha? Tito 2 yasema wanawake wazee wawe washauri. Soma watu waliopokea ushauri mbaya au mzuri kwenye Neno Mungu.

Je, Hekima ni nini? Someni Efeso 5 :22-24 na kujadiliana: Kumtii mume kuna maana gani katika kupata ushauri wa wengine? Je, mke afanyeje mume wake anapompa ushauri usio na hekima kama Abigaili?

Nakumbuka ushauri alionipa mama yangu kabla ya kumaliza darasa la 12 alipoona watu wanakuja kuulizia posa au uchumba. Hata niliposoma kwenye seminari kwa vile nilikuwa msichana peke yangu, na hata chuoni kwenye kitivo cha kemia nilikuwa ni msichana pekee. Na huu ulikuwa ni umri wa watu kutafuta wasichana wa kuoa. Wavulana waliokuja mama alinishauri: "Unaona watu wanavyokuja wengi sasa angalia usiwe na majibu ya dharau au jeuri, hata kama sasa unasoma na hutaki kuolewa, wajibu vizuri na kwa heshima, hata wale unaofikiri hawastahili kwa vile wana tabia mbovu. Waambie wakupe muda kufikiria jambo hili, na baada ya siku chache waambie kwamba upo shuleni bado, au una mambo fulani ya kukamilisha hivyo waendelee tu kwani haitawezekana." Akasema pengine baada ya miaka michache utakuwa umebadili mawazo, na kwa vile ulikuwa umewajibu kwa wema tu wanaweza kurudi na ukapata mtu mzuri wa kukuoa. Na hata isipokuwa wao, watakuzungumza vizuri kwa watu, na wale watu wataamini unajali watu.

Dunia inabadilika, leo wanataka kuoa, wewe hauko tayari, kesho utataka kuolewa nao watakuwa hawako tayari kwa sababu ya dharau au majibu yako. Kisha akasema si kazi ya msichana kumkimbiza mwanaume kama mke wa Potifa, wanaume wakufuate wewe, wale wanaokufuata ndio unamchagua mmoja kati ya hao. Ni aibu kumfuata fuata mwanamume, hata ukiwa unampenda, mwache akufuate. ingawa siku hizi wasichana ndo wanakazana sana kutafuta!'. Mwanaume aliumbwa ili atafute, na anajisikia vizuri akiona amempata, msichana au ametia bidii.. Zaidi ya yote, kuombea kupata mume bora hata zaidi ya mara tatu kwa siku ni muhimu maana hakuna ajuaye anayefaa. Wale walionekana wa kihasara, wamekuwa waume bora, na wale walioonekana wema, wamekuwa makatili kwa wake zao, moyo ni mdanganyifu, una magonjwa ya kuficha, ni nani aujuaye isipokuwa Mungu tu? Basi msichana ajue mume bora ni Bwana anayetoa, na si yeye kwa maarifa yake atampata.

Watu hubadilika, wale walioolewa na watu wa kufaa au 'stable,' wale watu walibadilika wakawa wabaya kwa wake zao, na wale tulifikiri walipata watu wasiofaa, wamebadilika. Mwenzi wa mtu aweza kufanya tabia yake ibadilike kwa kumpa nafasi ya kukua. Angalia zaidi kwenye Biblia wazazi walipotoa ushauri.

Je, binti anakufuata umpe ushauri kwenye mambo ya kawaida na nyeti? Je anakubali ushauri wako kuhusu marafiki zake au anabishana? Je, anafikiri mara zote yupo sawa? Je, anaomba ushauri wa mambo ya kiroho? Je, anatafuta kujua mapenzi ya Mungu kwa kusoma Neno lake? Je, anafurahia mashauri ya Mungu na wale wanaompenda Mungu, au anataka njia zake tu?

Kwa vile tuko katika jumuiya ya waumini, ni vyema tutiane nguvu na wale ambao tunaamini sawa. Tuwahusishe mabinti zetu na kanisa na kujadili mahuribi,

na Neno la Mungu pamoja. Mabinti zetu waone thamani ya kusaidia shughuli za kanisa. Waweze kusaidiana na shemashi kusafisha kanisa. Wawashukuru walimu wao wanaowafundisha kanisani na viongozi. Kuna huduma nyingi kanisani, za kusaidia wenye mahitaji; mabinti zetu waweza kujumuika

Mabinti zetu wajifunze jinsi ya kukaa kwa utulivu kanisani na kutunza siku ya Bwana kwa mpango wa Biblia ulioagizwa. Je, wanawake wa Agano la kale na jipya walikuwa na sehemu gani katika kanisa?

Je,analalamika kwenda kanisani na kuepuka? Je, anatokatoka kanisani kwenda chooni au kunywa maji kila mara? Je anatumia yaliyofundishwa kanisani? Je anaomba akila tu, bali haombei maisha yake ? Je, marafiki zake wa karibu ni wa kanisani? Je, anafurahia kuwa katika nyumba ya Bwana? Je, anaweza kusema alichofundishwa leo? Je, anahudumia wengine na talanta alizopewa? Je, anasikiliza kwa makini? Je, anaombea mahitaji ya mwili wa Kristo? Je anajua karama zake za Roho? Je, anawapenda (admire) wanawake wa kanisa lake au viongozi au anawapenda watu wa dunia (celebrity)?

"Huona kama bidhaa yake ina faida; taa yake haizimiki usiku;" fungu la 18 . Mwanamke wa huyu ni mvumilivu, (perseverance). Kama wazazi tuepuke majaribu ya kuwakinga watoto wetu wasipate shida au mambo magumu. Watoto wasipate kuona toka kwetu kwamba Mungu anawatendea visivyo haki. Tuwasaidie wamrudie Mungu na Neno lake. Tusiwapunje watoto wetu nafasi ya kuona ukuu na uaminifu wa Mungu katika shida zao ili wakue na kusafishwa kuwa vito safi. Vitabu kama Pilgrims progress ni vizuri kuona hili. Wawaulize wazee wa imani uaminifu wa Mungu katika maisha yao. Waebrania 11 ni sura ya kusoma na kujadili watu hawa jinsi walivyotatua shida zao wakisaidiwa na Mungu. Tunapokuwa na wakati mgumu, ni nini kibaya kitatokea? Ni nani anashika hatamu za mambo yote? Kutii na kuamini kunasaidaje kuwajulisha wengine kwamba Mungu ndiye Mweza.

Soma maisha ya watu mashuhuri ambao hawakukata tamaa wakati wa dhiki kuu au kufeli. Someni zaburi, na magazeti kama 'Voice of matyr' kwenye computer ya watu waliokufa kwaajili ya imani siku za karibuni. Someni Isaya 53. Je, ni watu gani kwenye Biblia walistahimili mpaka mwisho? Je tunawezaje kushukuru kwa kila jambo? Jadilini ukuu na uwezo wa Mungu pamoja. Je kwanini Mungu anaruhusu majaribu na mateso? (1Petro). Je, ni kwa jinsi gani mke anaweza kuwa mvumilivu na mtiifu kwa mume ambaye ni mgumu kuishi naye? Je, Biblia inasemaje kuhusu talaka? Talaka na uvumilivu zinahusianaje?

Je, anakata tamaa haraka na hataki kujaribu tena kama alishindwa? Je, analalamika na kujihurumia kama mambo hayaendi anavyotaka au mtu amemkosea? Je, anaweka akili yake kwenye matatizo tu? Je, anaweza kutalawa hisia zake wakati wa shida au akiwa ana matatizo bila kuwa na chuki? Je, anajionyesha kwamba ni yeye tu mwenye matatizo duniani? Je, anapata faraja ya maandiko akijaribiwa au akiwa na shida? Je, anajihoji kwa dhambi zake akiwa

na shida, ili aone pengine Bwana ataka kumrudi? Je,anajua kwamba Mungu anataka ajifunze katika shida zake? Je, anampa utukufu Mungu kwa jinsi anavyokabiliana na shida? Je,anamtumaini Mungu, na kuona majaribu yanamsaidia akomae?

''Hutia mikono yake katika kusokokota. Na mikono yake huishika pia. Huwakunjulia masikini mikono yake; naam huwanyoshea wahitaji mikono yake;'' fungu la 19-20. Mungu ametukarimu na anatualika nasi tukarimu wale tusiwaowajua, na kuonyesha upendo kwao. Mwanamke anajifunza ukarimu kwao, anapokuwa mdogo. Nyumba inayokaribisha wale wanaohitaji faraja, ushirika, msaada, na upendo ni nyumba ya mfano bora. Mama ataleta hali ya furaha katika kushiriki kusaidia wengine. Wengi twaambiwa wamekaribisha malaika bila kujua (Waebrania 13).

Tufundishe watoto kuwa wakarimu, kwa kupeleka chakula kwa wagonjwa, kusaidia wenye mahitaji kama wazee na wagonjwa, kualika watu nyumbani mwetu. Wafundishe watoto jinsi ya kumsalimu mgeni akija, kumtambulisha, kupokea mizigo yake, kuzungumza naye, kumhudumia chakula, na kumfanya ajisikie huru (ease). Jadilini, yeye kama mwenyeji afanye nini? Je, awezaje kusaidia familia kwa mgeni asiyetegemewa? Je, awezaje kusaidia watoto wa mgeni waliokuja kuwatembea na mama yao? Fikiria mtu ambaye mkienda kwake anawakaribisha kwa furaha na jaribu kumwiga.

Je, wageni wanaokuja kanisani awezaje kuwakaribisha wasikie wamependwa? Someni mifano ya waliokaribisha wageni kwenye Neno la Mungu. Je ni nani alikaribisha malaika? Angalia mifano ya Martha na Mary kwenye Liuka 10 na Yohana 12. Je, anaweza kupika chakula rahisi kwa upesi na kuwapa wageni? Je, anajua chakula wanachopenda watoto? Kwa wageni wanaolala, aweza kusaidia? Je, kuna tofauti gani kati ya mke na mume kwenye kukaribisha wageni? Je, anakaa na wageni au anajitenga

Je, yupo tayari wageni watumie vitu vyake? Je, anaingilia mazungumzo ya watu wazima kwa adabu? Je, anajitahidi kuanzisha mazungumzo na mgeni? Je anajaribu kuwa mkarimu kwa wageni hata wasio wa umri wake. Je, anasaidia wageni wajisikie wapo 'nyumbani''? Je, marafiki zake wakija anachukua jukumu la kuwakaribisha na kuwahudumia? Je!, ana adabu akikaa kwenye meza kuzungumza na wageni? Je, anawakirimu wageni wa kanisani na kuwasalimia? Je, anachukia wageni wakija kwa vile atakuwa na kazi nyingi? Je, anajua kwamba ukarimu wake ni jinsi ya kumhudumia Mungu? Je, anaona nyumba yao ni gurudumu la kufikia watu wamjue Mungu?

Kwa upande mwingine ajue jinsi ya kuwa mgeni bora, anapotembelea wengine. ucheshi, na kuwa na adabu pale alipo. Kuvaa nguo kwa heshima, hata kama ni wakati wa kwenda kulala. Jinsi ya kujibu watu au kufanya mambo kwa hekima. Mfano akisikia wenyeji wake wanagombana afanyeje? Shughuli gani aweza kumsaidia mwenyeji wake

Kuwa mwanamke mwenye rehema ni muhimu. Kusaidia masikini, kutia watu matumaini kiroho na kimwilli ni muhimu. Amhurumiaye Masikini, humkopesha Bwana, na Bwana hulipa bila kupunja. Watoto wa Mungu si mabahili bali hutoa. Mfundishe kutoa vitu vyake vya michezo, nguo zake n.k.

Pangeni jinsi ya kusaidia wajane, wagonjwa, vilema, wapweke, yatima, au wazee kanisani mwenu. Jinsi ya kuweka kando pesa za kusaidia wenye mahitaji; mfano walio jela, wamishonari, wanaotunza wagonjwa, wajawazito, watu wenye maradhi ya akili, watu waliodhulumiwa n.k. Je, mnaweza kuwasaidiaje? Je mafungu ganiya Neno la Mungu yatakuwa faraja kwao? Angalia www.persecution.com.

Soma vitabu vya injili na angalia jinsi Kristo alivyosaidia wenye mahitaji . Alisaidiaje masikini, wagonjwa, wajane au yatima. Soma gazeti au sikiliza taarifa ya habari na kuona mtasaidiaje waliopata maafa. Je, waweza kusaidia majirani zako ambao ni masikini bali hawatakiwi kupewa vitu bali ajira? Huruma au rehema in maana gani?

Je anaona watu wanapoteseka, au wanapokuwa na mahitaji? Je, ana huruma na mahitaji yao? Je, anapata huzuni na kuonyesha rehema kwa wahitaji? Je, anajua kusema maneno ya faraja kwa wale wenye maumivu? Je, anatoa muda na mali yake kwa kumpenda Mungu au atoa ili watu wamwone? Je, ana shauku ya kumfuata Kristo kwa kuhudumia watu? Je, anafurahi kuhudumu? Je, anajitoa kwenye huduma za kujitolea?

Twapasa kuhusika kwenye kusaidia mahitaji ya watu ya kiroho pia. Kama wanawake twahusika na haya kila siku. Tumeamriwa kwenda dunia yote na kuwaambia watu habari njema. Ni vyema aelewe kwa ufupi jinsi ya kutoa ushuhuda. Je, alikuwaje mkristo; n? Mungu amebadilishaje maisha yake. Ajue kisa cha msalaba hata kwa ufupi; kwamba wote tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu Warumi 3:23 na 6:23. Mshahara wa dhambi ni mauti, tunaokolewa kwa neema tu. Mungu anatupa neema tukiamini; ni lazima tuungame dhambi zetu na kuwa na toba ya kweli, tumwamini Kirsto kama Mwokozi wetu na tuna uhakika na Wokovu.

Je, aweza kumsimulia rafiki wokovu maana yake nini? Je, aweza kuomba na mtu na kumsaidia kuomba toba ya kwel? Aweza kuwa na klabu ya Bibia kwa watoto wa jirani? Watu walisaidia mahitaji ya kimwili ili kumsaidia mtu kiroho. Je, aweza kuchangisha pesa kwa mradiya kusaidia mahitaji ya kanisa,kama ujenzi?

Je, anaamini kuwa Yesu alikufa na kufufuka ili alipie dhambi zake? Je, amemkubali Kristo kuwa Mwokozi na Bwana wake? Je, anaumia kwa wale wanaopotea bila kumjua Mungu? Je, anawaombea wasiomjua Mungu? Je, anajua mafungu ya kumwongoza mtu kumwamini Mungu? Je, anaona aibu kumkiri Kriso kwa wengine? Je, anapenda kumtii Mungu? Je, maisha yake yaendana na Neno?

Je, anaombea watenda kazi wanaomtumikia Mungu na kuwatia moyo? Je, anatoa alicho kusupport kazi ya Mungu au anafikiria maisha hapa hapa tu?

Kuwa mtu wa haki ni moja wapo ya tabia ya mwanamke bora. Ni vyema ajue mambo yahusuyo sheria za nchi. Kupiga kura na kuheshimu viongozi. Ajue viongozi wanawekwa na Mungu na ni muhimu watende haki. Je, amchague nani anapopiga kura? Kuna ajenda nyingi mkristo anazopaswa kufikiria: Kama kutoa mimba, kuua wagonjwa (euthanasia), kuhukumu kunyonga, ushoga, ponografia, kutoza kodi, uasherati au uongo. Je, mtu anayempenda Mungu ahusikaje na hizi? Je, anapopiga kura ampigie kura viongozi anayeunga mkono haya? Je, kuna viongozi wanaompenda Mungu walioleta baraka kwa watu? Soma maisha ya Daniel, Nuhu, au Rehoboamu.

Je anajua viongozi wake, na anajua mamlaka yana maana gani? Je, anaweza kutoa hoja yake kupeleka kwenye uongozi wa ngazi za chini na hata juu? Je, anajua jinsi mswaada unavyokuwa sheria? Anajua mambo yanayoendelea nchini sasa hivi? Je, anaweza kugundua maneno ya yanayoposha ya "mawazo ya binadamu" kwenye vyombo vya habari? Je, anaonyesha heshima inayoakiwa kwa viongozi wa serikali, hata wale wanye ubinafi na uovu? Je, pale alipo anajitahidi kubadili sheria mbovu kwa kuzungumza na viongozi mahalia? Je, anahudumia majeruhi waliokosewa haki? Je, anajua kwamba mamlaka youte imewekwa na Mungu?

" Hawahofii theluji watu wa nyumbani mwake, maana wote wa nyumbani mwake huvikwa nguo nyekundu;" fungu la 21.

Mwanamke hodari hujihami na wakati ujao. Ni vyema binti ajue simu za kupiga za dharura, kama vile ndugu wa kuomba msaada, polisi au zima moto. Yusufu alitayarisha Misri kwa wakati wa shida (Mwanzo 41). Nasi pia tuwafundishe watoto wetu kufanya hivyo. Tuwafundishe kujua cha kufanya moto ukianza kutokea, pa kukimbia na jinsi ya kusaidia wadogo zao. Ajue tochi, vibiriti au mishumaa vilipo.

Ukimwachia alee watoto wadogo, mfundshe vizuri jinsi ya kuwachunga na hatari zinazoweza kutokea na anavyoweza kuzikabili. Je, kuna majani au maua ya sumu karibu? Je, mtoto akinywa mafuta ya taa au akizama kwenye mto afanyeje? Mhoji mama ambaye amekutana na matatizo ya hatari za watoto nyumbani, alifanyeje? Mfundishe binti hatari za maji, umeme na gesi, na jinsi ya kuzima inavyotakikana.

Huduma ya kwanza ni muhimu; kila mtoto afundishwe kwa uwezo wa umri. Je, mtoto akiugua ghafla anajua cha kufanya, na mtu wa kumwuliza na kisha ampeleke mtoto hospitali? Je, sehemu mnayoishi ina hatari za aina gani, ni yapi mfanye mkiishi hapa? Je, anaweza kujua chakula kimeharibika na cha kutupa kisije kikasumisha watu? Je, mabaki ya chakula ni ya kutupa? Je, nyama, Mayai au samaki zinatunzwaje?

Je, mshikio wa sufuria hugeukia upande gani?, unapompa mtu kisu ushike upande gani? Je, anajua jinsi ya kutumia presha cooker kwa usalama? Mfundishe jinsi ya kutunza mboga kwa usalama, kwa kukausha au kuweka kwenye chupa. Ajifunze machache ya usalama kwa vyombo vya usafiri kama vile baiskeli, pikipiki au gari. Je, aweza kubadilisha matairi? Je, anajua jinsi ya kupata chanjo bila kudhurika? Mfanye utafiti wa pande zote.

Kitabu kama "Mahali pasipo na Daktari" ni kizuri, kuwa nacho. Ni wakati gani huduma ya kwanza ya nyumbani haisaiidii na lazima mtu apelekwe hospitalli? Jifunze na binti tiba mbadala na kukuza mimea ya tiba (herbs for medicine kama vile echinecia, tangawizi, vitunguu saumu) .Chukueni madarasa ya kuokoa mtu majini, kujilinda (self defence class). Jifunzeni usalama wa kuwa/kutokuwa na silaha mbali mbali nyumbani, kama mishale, rungu, mitego ya panya au sumu za panya au bunduki.

Je, anajua wakati wa tahadhari kama haupo? Je, anajua kuogelea? Je, anaweza kuwa na upeo wa kuona hatari inayokuja? Je, anakuwa mwangalifu ili asiwe hatari au kuumiza wengine? Mfano kuacha maji bila kudeki, kurusha vitu, n.k. Je, akiharibikiwa na chombo cha usafiri anaweza akawa msaada? Je, anajua jinsi ya kukabiliana na dharura ya nyumbani? Je, anashughulika na chakula kwa usafi na usalama? Je, anajua cha kufanya endapo tetemeko, au dhoruba ikitokea? Anaweza akatumia vyombo vya kazi kwa usalama? Je, anajua kujikinga na maradhi? Je, anajua kujikinga na mtu anayetaka kumpiga? (self defence moves), Je, anamtumaini Mungu kama kinga yake kuu na mpaji?

"Hujifanyia mazulia ya urembo, mavazi yake ni kitani safi na urujuani;" fungu la 22.

Mwanamke anayemcha Mungu anapenda vitu vya kupendeza pia, anajitahidi ashone na kujua ustadi fulani. Anajitahidi katika kuvaa vizuri hata nyumbani, asiwe kama yule anayekimbiza ndege shambani, avaaye vizuri akitoka nje ya nyumba. Ajifunze kutandika kitanda chake na kuacha chumba chake katika hali nzuri akiamka. Chumba kinabadilika kabisa, kwa kutandika tu kitanda! Aweza kusaidia kufuma vitambaa vya viti na meza. Kupanda maua na kuweka nyumbani, kusaidia ndugu zake kushona vifungo. Mungu ametuumba tupende ustadi na nakshi. Mfundishe kushona, kukarabati nguo , kama huwezi mtafute mtu amsaidie. Ajifunze kuweka zipu, kushona begi, kushona kitambaa cha mkononi, nguo ya mtoto, sketi, apron. Mwaweza hata kushona na kusaidia wenye mahitaji. Kuhudhuria madarasa ya ushonaji, upambaji, ufumaji kupata maarifa zaidi. Kina mama waweza kufundisha haya kwa wasichana kwenye nyumba za ibada au jumuiya. Vitabu kama "Simple secrets to a beautiful Home;" by Emilie. Barnes, ni vyema kuwapa wasichana wetu wavisoma

Je, chumba chake kina mpangilio? Je, anajaribu kukifanya chumba chake kuwa safi na maridadi? Je, meza, viti , nguo na matandiko yake yamekaa sawa? Je, anachukua muda kujifunza kupamba, kwa maua na vitu rahisi chumba,

nyumba au hata kushirikiana na wengine kulipamba kanisa la Mungu? Je, mapambo yake ya kuta ni ya picha za watu wa dunia na celebrity na magazeti ya watu wa anasa, au ni mambo ya kumsaidia?

Yaonekana mwanamke huyu anavaa kitani na zambarau, hizi ni nguo za kifalme, ni binti wa mfalme huyu! Nafikiri kama tuna uwezo tuwe na nguo chache nzuri, na pia kusaidia wenye mahitaji. Kuwa mtoto wa mfalme ni pamoja na tabia ya kifalme. Mabinti zetu wajifunze tabia za adabu na upole za kifalme. Kusema asante, tafadhali, samahani, pole ni maneno ya dhahabu au kifalme. Wajue jinsi ya kuwa watulivu kanisani na kwingineko; na si kupayuka payuka na kuongea kwa sauti ya juu, au kubishana. Wajue jinsi ya kumwita mtu au kuzungumza na mtu. Wajue sheria (rules) wanapotembelea watu wengine. Gary na Cathy Maldaner wameandika kitabu "Visiting other families in polite moments". Jaribu kuona ni mambo gani ya kufundisha watoto wajue mnapotembelea mtu (ugenini).

Je, mnapoenda kwenye hoteli au mgahawa mfanyeje (polite manners). Jinsi ya kuserve chakula, jinsi ya kuomba menu, kutumia kijiko au uma, au napkin (karatasi ya kujifuta mdomo). Andikeni sheria hizi mahali na kujifunza pamoja. Mfano ni nani anaanza kuserve chakula mkiwa wageni mahali? Vitabu kama Manners made easy by June Hines Moore ni msaada.

Jinsi ya kujibu simu, na kujitambulisha unapokutana na watu. Jinsi ya kumsifia mtu au kumtia moyo (compliment/praise), jinsi ya kumlaki mgeni mlangoni mwako, jinsi ya kushukuru ukisifiwa, jinsi ya kushukuru ukimaliza ukaribisho, jinsi ya kupenga makamasi, kupiga chafya au kukohoa mbele ya watu. Jinsi ya kutoa hudhuru ukienda chooni, jinsi ya kupanga meza na kupakua watu wale, jinsi ya kufanya mtu akusikilize anayefanya kazi Fulani (interrupting). Jinsi ya kuwa mgeni bora ukialikwa mahali, jinsi ya kutokuwa mchoyo na kutojifikiria, au jinsi ya kuandika shukurani kwa waliokualika ukirudi.

Je, msichana ajifunzeje jinsi ya kufanya mambo kwa tanashati (a girls guide to etiquette)? Someni vitabu vya injili, Je, unajifunza nini kuhusu Kristo kama mgeni, rafiki, mwalimu. Aliwasalimuje watu, alizungumzaje nao, aliaganaje nao, Soma jinsi Nabali 1Sam 25 na Hanuni 2 Sam 10; walivyokuwa na adabu mbaya. Je, wafilipi 2:2-4 inatusaidiaje kuhusu mahusiano na watu?

Andika list ya vile vitu vinavyowasinya watu (annoy) au ambavyo havionyeshi tabia njema (bad manners). Andika jinsi binti anaweza akabadili tabia hizi mbovu. Andika watu ambao ungependa kuwa nao, angalia tabia zao, Je, wana tabia gani za kiungwana (polite habits)? Je, wanaheshimu wengine kuliko wenyewe, linganisha na tabia yako. Angalia mfano wa mwanamke mwenye tabia njema muulize anafanyaje haya (graciousness and good manners/etiquette). Je, tunda la roho linahusikaje na tabia zetu Gal 5:22-23.

Alika mgeni kisha panga binti apange meza, aweke maua , apike na kuwa mwenyeji (gracious hostess). Angalia kwenye Neno la Mungu wale walioonyesha tabia njema, walifanya nini? Je, wapi biblia yatuambia tuwe na upole na utu

wema (politeness/kindness); kama kujali wazee au kuhudumu wengine kabla yetu. Je, kwa nini si vizuri kuzungumza ukitafuna chakula mdomoni?

Je, anawafanyia wengine vile anavyopenda kufanyiwa? Je, ana tabia njema akiwa mezani (manners), Je, anazungumza kwa kujali watu (politely)? Je,anajua kutoa udhuru anapotakiwa, Je, anapenda watu na ana tabia njema (good etiquette) akifuata sheria zake kwa unyenyekevu na upendo kwa wengine. Je, wengine wapenda kuwa kuzungumza naye au kumtembelea? Je, mara nyingi unapata aibu ukiwa na wageni wako kwa tabia au jinsi anavyozungumza na watu? Je, anaonyesha adabu kwa wazee? Je, anajua kutoa shukurani, na anaheshimu vitu vya watu?

Ni vyema kuwafundisha watoto kuwa na kiasi. Tuwafundishe kwamba wanavyovaa au kuzungumza waweza kukwaza watu. Tuwaambie jukumu lao kuwa na hekima katika kuvaa, na kuzungumza na watu. Lazima wajue wao ni watoto wa Mfalme, na kufundishwa tangia wakiwa wadogo. Tuwavalishe kwa style zinazofaa toka udogoni.

Mara nyingi watoto wa kike wadogo wanavalishwa nguo za wazi, kama vikaputura vifupi, na mtoto akifika miaka 12 tunaanza kumwambia hiyo haifai na ameivaa toka udogo! Watoto wadogo ni vizuri wavalishwe kaptura wakiwa na magauni, maana wakicheza nguo za ndani (chupi) zaonekana. Mtoto asitembee amefunga kanga iliyoacha mabega siku nzima, bali aongeze na nyingine ya kufunika mabega/kifua.

Tuwafundishe pia kuwa wanyenyekevu wenye kiasi, na wasiojisikia kwamba wao ndiyo muhimu kuliko wengine. 1Tim 2;9, yaeleza mwanamke anayempenda Mungu. Je,mavazi gani au fashion ambazo hazina kiasi? Lazima kuwe na jinsi ya kuvaa (dress code). Je, wanavaa suruali (trousers) za aina gani? Je, zinabana hasa kwenye sehemu za siri? Je, nguo zinaonyesha kifua na matiti? Je, magauni yako juu ya magoti? Mwambie binti azungumze na baba yake kuhusu nguo ambazo hazileti majaribu kwa vijana wa kiume au hata wanaume watu wazima.

Chukueni Catalog ya nguo za wanawake zenye picha na kuijadili. Kaeni mahali na kuona watu wanaopita na kujadili nguo ipi ni ya kiasi na ipi haina adabu (immodest). Je, unapima nguo hizi kutokana na kiwango gani? Andikeni sheria ya nguo za msichana anayemwakilisha Mungu, na jinsi ya kutengeneza nywele, kucha au uso kwa kumwakilisha Mungu. Je, mwonekano wa nje unajalisha au bora mioyo yetu ni safi hivyo inatosha? Ni kwa nini Mungu alitupa nguo bustanini mwa Edeni? Kwa nini hakuwaachia wakae na majani yale ya mikuyu waliojitengenezea yaliyowafunika kidogo tu na kuacha utupu mwingine? Kama Mungu alitupa nguo, ya kufunika mwili na si majani, hii ina maana gani kwetu?

Angalia fasheni ya nguo ya nchi mbali mbali, kisha angalieni miaka 50 hata mia ya nyuma watu walivyovaa. Je, hizi fasheni zinawakilisha maadili na

utamaduni wa watu hao? Binti ajadili na wazazi kwamba goli lake ni lipi katika uvaaji wake? Anavaa kumpendeza Mungu au wanadamu; na anataka watu wamwone au amletee Mungu utukufu?

Nchi nyingi siku hizi wana sehemu ambazo familia yote inaenda bila nguo kabisa (nude beaches, or recreation); kwa nini hili ni kosa? Kwa nini Nuhu alimlaani mwana wake aliyemwona uchi? Wakati Kristo yupo duniani watu walivaaje? Je, uchi ni nini?Je! Ni kutokuwa na nguo kabisa au kuvaa nusu nusu, sehemu zingine zikiwa wazi?.

Neno la Mungu liko wazi kuhusu sehemu za mwili za kuacha wazi na za kufunika. Mwambie binti aende na baba yake kununua nguo zake, na baba atoe mawazo kwenye uchaguzi, kisha aseme kwa nini amechagua nguo hiyo. Mwambie baba yake naye waangalie nguo zake kabatini na wazithathmini na kutoa sababu kwanini zinafaa au hazifai.

Soma mwanamke mgeni kama wa Mithali saba. Je, anafanya nini kuwavuta wanaume? Linganisha wanawake wawili wa ufunuo, yule aliyevikwa jua na mwezi na yule aliyedanganya mataifa. Tofauti yao ni nini? Wanaume wa namna gani waenda kwa wanawake wageni? Mwulize baba amweleze binti jinsi vijana wa kiume wanavyoona mwanamke akiwa na nguo imebana, au inaacha sehemu nyeti za mwili (flirtatious). Someni kitabu "For Young women only;" kilichoandikwa na Shaunti Feldhahn na jadilini wote nyumbani mwenu.

Someni Mathayo 5:27-28. binti anapovaa afikiri kuhusu wanaume watakaomwangalia na yale watakayofikiri. Fikiria mwanamke mwenye adabu na roho ya kicho (modesty in spirit and dress).Angalia tabia yake, matendo, na jinsi anavyozungumza na wanaume, au anavyovaa. Soma wanawake wasio na kicho na jinsi walivyovaa. Walifanya nini?, matokeo yake yalikuwaje? Je, kutovaa vizuri kwawezaje kuwa kukosa uaminifu kwa yule utakayeolewa naye? Je, inasaidiaje wavulana wengine kukosa uaminifu kwa wake zao watakaoa? Mtayarishe binti kwa uchumba atakapofikia miaka kama 18 hivi. Jadilini Jinsi ya kutokuwa mtu wa 'sheria' (legalistic) na uvaaji kwa adabu kikawa kimungu chetu.

Yasemekana wanaume wanajaribiwa kumtamani mwanamke na mwanamke anajaribiwa kumjaribu mwanamume amtamani. Jadilini hili. (Man is tempted to lust after a woman, and a woman lusts to be lusted after).

Je, anapenda ampendeze Mungu kwa uvaaji wake au anapenda ajiletee utukufu na watu wamwangalie? Je!, anapokea mashauri kwenye uvaaji au anajivalia chochote kinachomfurahisha? Je, anajua jinsi macho ya wanaume yanavyotazama mavazi na wanavyofikiri wanapoona mwanamke amevaa kwa namna fulani? Je, anawalinda wanaume wasiwe na mawazo ya dhambi kwa uvaaji

wake? Je, anavaa nguo zinazomfunika au anapenda kujionyesha mwili wake? (expose body

Je, anavaa kama msichana au anapenda avae kama mvulana? Je, anapenda kutongoza wanaume kwa uvaaji wake, tabia na maneno? Je, anazidisha kuvaa kwa adabu mpaka anaonekana vibaya na kama si msichana? (overdo modesty). Je, ana kiburi kwamba anavaa kwa adabu na anamjaji kila mtu anayevaa vibaya? Je, anakuwa mtu wa sheria 'legalistic' kwenye uvaaji wake, akishikilia mambo ya nje, bali ndani ya moyo wake kuna roho ya uasi? Je anaweka sheria zake za uvaaji mzuri kwa wengine? (impose legalistic starndards of dress o others).

"Mume wake hujulikana malangoni, aketipo pamoja na wazee wa nchi;" fungu la 23. Huyu mwanamume anayeheshimiwa malangoni, lazima awe anaheshimiwa nyumbani pia. Mithali 12:4. Mwanamke mwenye hekima anayemheshimu, anamsaidia mume kukomaa na kukua katika uongozi na kuchukua majukumu.

Kumheshimu mume, kunaanza msichana akiwa mdogo, kwa kumheshimu baba yake. Kutona tona (nagging) ni tabia ya kuepuka. Lazima ajifunze kuheshimu, na kuona baba na mama yake ni mamlaka yaliyowekwa na Mungu katika maisha yake. Ajifunze kuitika kwa adabu anapoitwa na baba yake, amsaidie baba yake kumpokea mlangoni, kuchukua koti lake, kumpikia chakula chake na kumtengea. Ajifunze kumshukuru baba yake, na kujua vile vitu vinavyomfurahisha, kama vile gazeti, muziki, au vitabu. Andika orodha ya vile vinavyomchukiza na kumpendeza baba yako.

Someni kitabu cha Mithali na kuona uhusiano katika ya mzazi na mtoto. Pia someni Efeso 5:33.

Je, ni kitu gani kinaonyesha heshima kwa baba yako? Je,mama anamweheshimuje baba? Hapa sisi wanawake lazima tujitahidi ili watoto wetu waone. Je, tunawasaidiaje waume zetu kama wasaidizi? Je, anawezaje kuonyesha heshima kwa babu yake au kaka zake? Je, mwaweza kuandika list ya vitu vinavyoonyesha kukosa adabu? Kama binti ana shida ya kuheshimu wazazi aandike sababu za kutowaheshimu, na kuona Biblia inasemaje kuhusu hizi sababu.

Soma yahusuyo mke wa Ayubu, Mikali, na Vashti, walikosaje heshima kwa waume zao? Soma Sara, na Esta waliheshimuje waume zao? Chunguza watoto au wanawake wanaokosa heshima kwa waume au wazazi wao. Je, watoto wanapata mfano gani kutoka kwa wanawake wanaokosa adabu kwa waume zao? Je, mamlaka ya mwanamume yanakuaje katika nyumba hii? Je, mamlaka ya Mungu yanakuwaje katika nyumba hii?

Binti ajadili na baba yake umuhimu wa kumheshimu mume. Je, mfanyakazi, raia, mtoto au mke afanyeje endapo mamlaka haijiheshimu? (unworthy of respect). Je, yuko huru kutiii mamlaka, hata inapofanya dhambi?

Je, anazungumza kwako na kwa baba yake kwa adabu? Je, anazungumza kwa maneno ya adabu kwa wazazi na kwa mamlaka? Je, unapozungumza naye

au kumwita anaitikia na kugeuza uso wake akusikilize? Je, uso wake na mwonekano anaonyesha anatii? (expressions, gestures, and posture). Je, anakuheshimu mbele ya watu na hata mkiwa peke yenu? Je, anasema madhaifu yako mbele ya watu wengine? Je, anakukosoa mbele ya watu? Je, anaheshimu watu wazima polisi na viongozi wa serikali? Je, anajitahidi akupendeze? Je, anakuona wewe kama mamlaka ambayo Mungu amemwekea katika maisha yake? Je, anaheshimu maoni yako? Je, anajua jinsi ya kukueleza pale anapotofautiana nawe? Je, anakukosea adabu na kuonyesha kwamba anaona aibu wewe kuwa mzazi wake? Je, anapenda kukukebehi au kukucheka mbele ya watu?

Kumsupport mume ni muhimu sana, hebu wasichana wafundishwe. Hii inafanya waume zetu kufanya shughuli yao ya uongozi waliyopewa na Mungu kwa ubora zaidi. Mwanamke ni msaidizi, wa mume wake, anapaswa kumtii na kutumia muda na uwezo wake kumheshimu mume wake. Akifanya hivi vyema aweza kuwa taji kwa mume wake. Pengine inabidi aweke kando matakwa yao ili kuwahudumia waume zao, na hili wajifunza wakiwa wadogo.

Pengine wanawake wengine hawafikiri hili, kwa vile wameolewa na wanaume wasiomcha Mungu, ila hata hao wanahitaji kuheshimiwa; Math 20:28. Hata mwana wa Adamu alikuja kutumikia watu. Hebu ajue jinsi ya kutumikia wadogo zake, dada au kaka zake. Amuulize mama yake au mama wengine kwamba "Magoli yako leo ni nini?" Ataona magoli ya mama wengi ni ya kuhudumu, na kutumikia nyumba zao.

Ajifunze jinsi ya kupendeza kaka zake, au dada zake kwa siku moja. Awaombee wazazi wake. Jadilini njia za kumsupport baba kwenye shughuli zake. Je, anajua kuacha anayopenda (interest) ili kusaidia wengine? Amwangalie mama yake aone anayofanya kumsupport baba yake. Msichana amhoji baba yake ni kwa njia ipi mama alimtia moyo katika mwito wake aliopewa na Mungu. Je, amemsaidiaje katika maisha yake? Angalia jinsi mabinti wanaowasaidia baba zao. Wahoji wanaume wawili jinsi wake zao walivyowasaidia kufanikiwa kimaisha? Ni jinsi gani wamewatia moyo kukomaa katika shughuli zao za uongozi?

Soma maisha ya watu mashuhuri na viongozi wa historia na nafasi ambayo wake, au mama zao walichukua kusaidia haya? 1Tim 3:1-13.

Je, mwanamke ana jukumu kumsaidia mume wake kwa namna gani? 1Tim3 na Tito 1 zinaonyesha kwamba mwanamume anahitaji mke kumsaidia kwa mambo mengi. Angalia mfano wa Yesu kama mtumishi, alitumikiaje watu?

Angalia wanawake kwenye Biblia kama Sarah na Priscscilla walivyosaidia waume zao? Soma maisha ya wake kama wa Lutu, Haman, Yezebeli au Herodias; Je, walisaidiaje waume zao? Angalia familia ambayo mke hataki kumsaidia mume wake, je, matokeo ni nini? Je, kwa wale wake wanaotaka kuwa na taaluma na

kuiendeleza badala ya kusupport waume wao, jiulize jinsi itakavyowasaidia watoto au waume zao.

Je, familia yawezaje kufanya dhambi kama timu? Je, mke anawezaje kuwa msaada kwa mume wake kwa maneno yake, kwa kumsifia yale mema yake, kwa kuwa mnyenyekevu na kuwa mwenye heshima, au kuwa maombi? Andikeni njia 15 za kumheshimu mume. Je, Jukumu lako kama mke lawezaje kuwa kama kanisa, msaidizi wa Kristo kwa mume wako?

Fungu la 24 latuonyesha ujasiliamali ambao mabinti zetu wanatakiwa wajifunze. Tufundishe mabinti zetu jinsi wanavyoweza kujiajiri wenyewe majumbani ili kuwa na kipato na ustadi. Baba au mama waweza kubuni mradi wa kusaidia, pengine kuuza vitu vidogo vidogo kama maji, vitu vya kushona au vya kupika. Kama kuna kazi anazoweza kuzifanya na kulipwa afanye vile.

Wanawake kama wale wa Matendo 16-15 wanatuonyesha kwamba wanaweza kuuza vitu vya nakshi. Jadilini faida za mwanamke kuwa na kazi za kumletea kipato nyumbani badala ya kufanya kazi nje ya nyumba. Jifunzeni yahusuyo leseni ya biashara na kodi ya serikali. Hoji wanawake wenye biashara zao, Je, wanafanya nini? Fikiria biashara inayohitaji mtaji mdogo na muanze. Je mwanamke atumiaje mapato yake anayopata kwenye kazi zake?

Je akifanya kazi ina ubora? Je anapenda Mungu afurahi na kazi yake? Je, anaongeza ustadi wa ufundi alio nao? Je, ana ustadi wa kumwezesha kupata kipato? Je, wengine wanajua ni mfanyakazi bora? Je, watu wanapenda bidhaa zake au ustadi wake? Je, ana mbinu za ujasiliamali? Je, anapenda kufanya kazi nje na nyumbani? Je, akiona hitaji anajaribu kulitatua? Je, anapenda apate pesa kwa mahitaji yake binafsi tu au kusaidia familia na wengine pia?

"Nguvu na hadhi ndiyo mavazi yake, anaucheka wakati ujao;" fungu la 25. Mwanamke huyu anajua maisha ya imani, kuridhika na kumshukuru Mungu. Anajua Mungu ameshika hatamu ya wakati ujao. Twahitaji kuwasaidia mabinti kuridhika na yale ambayo Mungu, na sisi wazazi tumewapa. Twaweza kujadili na kuandika pamoja yale ambayo tunashukuru kwayo. Je, anawashukuru wazazi wake kwa yapi? Kuna tofauti gani kati ya kuomba na kushukuru? Filipi 4:6-7 na 1 Thes 5:16-18. Je, wivu, chuki,

Soma watu ambao hawakuridhika kwenye Biblia. Kila mara unapojaribiwa kulalamika, soma Wafilipi 2 na Isaya 53. Je, binti ya Mfalme anapaswa kuishi maisha ya kutoridhika? Zungumza na mwanamke mtu mzima kuhusu kuridhika. Jadili neno kutamani (covet) lina maana gani? Andikeni orodha ya vitu ambayo hamridhiki navyo (discontent); kwa mwonekano wako, unapoishi, familia yako, kisha andika shina la kutoridhika na hivi vitu kwenye moyo wako. Kisha ungama kwa Mungu. Angalia Waebrania 11, na jinsi kila mtu aliyeandikwa alivyoridhika.

Je, anamshukuru Mungu kwa anayompa? Je anadai kununuliwa vitu mkiwa dukani? Je, anajali kama mwingine atapata sehemu kubwa kuliko yeye? Je, anataka kuwa na vitu vile anaona wengine wanavyo? Je, anaweza aishi maisha magumu na kuona mafundisho Mungu anampa?

Je, anamtegemea Mungu kama mtoaji? Je, anakazania mambo ya kupita au ya milele? Je, anaridhika na alivyonavyo au anataka zaidi? Je, ana roho ya shukurani kwa wazazi na upendo wenu? Je, anatoa shukurani kwa huduma au anavyofanyiwa? Je, anapenda kulalamika na kulialia? Je, anajitahidi na wengine kupata anachotaka? Je, anapenda kutetea haki zake mara zote? Je, anajihurumia kupita kiasi; (self pity)? Je, anatamani vitu vya wengine na kupata wivu? Je, anatamani talanta au kufanikiwa kwa wengine? Je, anatamani baraka za wengine na zinamtia uchungu?

Mungu hutoa mahitaji yetu sasa na ya wakati ujao. Ni nani alimpa Adamu mke wake? Je, Mungu ataka tuwe watu wa namna gani? Mika 6:6-8. Angalia wanawake wote waliosaidia kazi Yesu au mahitaji yake, wangapi walikuwa hawajaolewa? Wajue wanawake ambao hawajaolewa kwenye ushirika wao na kuwatembelea. Je, binti anaweza kuifanya miaka ya kutoolewa iwe bora (shule, kusoma Bibia, huduma, kukariri mafungu, ustadi). Je! Anajua dhambi iliyoingia ya wanawake kuolewa na wanawake na wanaume kuolewa na wanaume? Jadili naye.

Biblia yataja watu kama vile Miriamu, Rahabu, Delila, Mariamu, Martha, Esta, Ana, mjane wa Serepta, binti za Zelofehadi. Je, kutoolewa kwao kuliwasaidiaje kutumika walivyotumika? Je, Mungu aliwasaidiaje kupata riziki? Makosa gani walifanya? Na adhabu gani waliyoipata? 1 Kor 7:34-35.

Andika jinsi ambavyo mwanamke asiyeolewa na asiyekuwa na jukumu la kumpendeza mume anaweza kuhudumu kwa ufanisi mkubwa. Angalia jinsi uhuru wake unavyoweza kumsaidia kuwa wa huduma kwa kazi ya Mungu. Ni mambo gani ambayo waweza kusaidia kanisa sasa ikiwa haujaolewa? Je, ukiitwa na Mungu kutoolewa (single) waweza kumtumaini Yeye?

Zungumza na wazazi kuhusu kuitwa kumtumikia Mungu pasipo kuolewa. Kwa nini Mungu, wakati mwingine huita watu ambao hawajaolewa? Je, watu hawa wanajisaidiaje kupata riziki? Je, usipoolewa utaishi kwenye mji wako mwenyewe? Je, ni wapi utaomba ushauri ukiwa mwenyewe (single)? Soma Biblia inapozungumzia: "Mwito wa kuishi maisha ya usela/solemba; (single). Soma kitabu; 'Did I Kiss Marriage Goodbye;' cha Caroly MCCulley. Je, maisha ya kuishi mwenyewe yanaweza kuwa bora na kamili? Jadilini kuhusu upweke.

Je, anamtumaini Mungu kwa kila jambo na anaridhika (fulfillment) na uhusiano wake na Mungu? Je, anajua adui anakuja kwa njia nyingi zaidi ya ile ya kutenda dhambi? Kukata tamaa, unafiki, marafiki wabaya, kuchoka; n.k. Je, amejitoa kwa Mungu kutumikia wengine, na anatumia nafasi hiyo kuanzia

nyumbani? Je, ana nafasi nyumbani kujifunza kuwa mke na mama? Je, anamtumaini Mungu kumchagulia mume na anayefaa kwa wakati unaofaa, kama ndio mpango wake? Je, anajali mawazo yako kuhusu wavulana wanaokuja kwake? Je, anajali mambo ya kuolewa kuliko utii kwa Mungu? Je, ana ndoto za mchana kuhusu ndoa? Je, ana mawazo ya mahaba yasiyofaa?

Je, kipi ni muhimu kwake, kuwa mcha Mungu aliyekomaa au kuolewa na mtu yoyote? Je, anaona wivu rika zake wakiolewa? Je, anapata hofu akijua hataolewa? Je, anajua kwamba Mungu anaweza kuwa amempa wito wa useja na kumtumikia badala ya kuolewa? Je, anajua kwamba Mungu ana mipango maalumu naye, endapo akiolewa au asipoolewa? Je, anatumia miaka ya kutoolewa ni ya kujitayarisha kwa wito mkuu wa Mungu? Je, anazungumza na wanawake wasioolewa kanisani kwa njia nzuri na upendo? Je, ana upendo wa kutaka kushugulikia mahitaji ya wale wapweke?

Tufundishe mabinti zetu kutoishi maisha ya hofu, bali nguvu na ujasiri. Watambue kuomba ni muhimu. Wanapopata hofu wamtegemee Yeye. Someni kuhusu ahadi za Mungu na ulinzi wake. Angalia wanawake hawa walimtumainije Mungu, mke wa Nuhu, mke wa Lutu, Sara, Esta, Yokebedi, Debora au za Ruth. Chagua Zaburi za kusoma pale unapokuwa na woga. Angalia pale wana wa Israeli walipopata hofu kwenye kitabu cha Kutoka. Je, wale wa Waebrania 11 walionyeshaje ujasiri?

Wahoji wanawake kadhaa pale walipojaribiwa kuwa na hofu na ilikuwaje walipoogoa na ilikuwaje walipomtegemea Mungu? Soma maisha ya Sara, mazuri na madhaifu yake yalikuwa yapi? Je, alifanyaje alipojaribiwa? Je, kwa nini ametolewa mfano kwa wale wenye imani?

Je, anahofu ya kumtumaini Mungu kumtunza? Je, ana imani ya Warumi 8:28? Je, anajua mafungu ya kusoma akiwa na woga? Je, akiwa na woga anaomba? Je, anaogopa kujaribu chochote kipya? Je, anaogopa watu wanavyomfikiria? Je, anaogopa kufanya makosa? Je, anaogopa wakati ujao (future)? Je, anaweza kusema 'hapana' watu wakimwambia atende uovu? Je, anaogopa kujeruhiwa? Je, anaogopa kuzungumza na watu? Je, ana wasiwasi, na kuona kwamba atashindwa, na kuona matatizo tu?

Je, ana ujasiri wakutatua magomvi au kutoelewana na marafiki, ndugu, walimu au wazazi? Je, ana ujasiri kusema alikosea? Je, yupo tayari kuomba msamaha akimkosea mtu? Je, anamwogopa Mungu zaidi ya binadamu? Je, anaweza kumwambia rafiki akifanya dhambi? Je, anakata tamaa afanyapo dhambi? Je, anapokea maonyo na kukosolewa kwa hali chanya? Je, anaogopa kutoa mawazo yake? Je, anaogopa kumshuhudia Kristo mbele ya watu? Je, ana hofu kuelezea hisia zake?

"Hufumbua kinywa chake kwa hekima; na sheria ya wema i katika ulimi wake." Ulimi hauwezi ukafungwa, una uovu usiotulia. Umejaa sumu iletayo mauti. Kama wazazi twapaswa tuwasaidie watoto 'kufuga' ulimi mapema ili wawe mibaraka kwa waume zao, watoto, kanisa na jumuiya. Daudi anamwomba Mungu atie kufuli ulimi wake. Ni vizuri tuwaambie mabinti zetu pale wanapozungumza isivyo, na marafiki zao waweza kuwa walinzi wao pia. Twapasa tusirudishe ubaya kwa ubaya. Twawezaje kufanya hivi? Mwambie binti amuulize mtu amwangalilie yale maneno yote yasiyo na sababu (idle words ya Mathayo 12:36-37).

Someni Yakobo 3 pamoja na kujadili. Soma watu ambao wamewasaidiwa kwa maneno mazuri, na wale ambao maneno mabaya yamewaharibia. Angalia maneno kama magomvi, malamiko, umbeya, uongo, kutia chumvi, kushuhudia uongo, na kukufuru.. Je, mwanamke anawezaje akajitawala kwa maneno yake? Soma kisa cha Abigaili au mke wa Pilato. Je, mwanamke awezaje kuwa na maneno ya kutia moyo au ushauri mwema? Twawezaje kutawala nafsi tunapozungumza? Twawezaje kufanya mazungumzo yetu yakawa mbaraka (improving speech)?

Je, anapenda kuwabandika watu majina? Je, anazungumza kwa ujinga, kwa sauti inayokera? Je, anatania wengine(mock)? Je, anapenda kulialia na kulalamika? Je anapenda kusengenya wengine? Je, sauti yake inakuwa kali wakati wote? Je, anapiga mayowe akigombana na nduguze? Je, anapenda kuripoti makosa ya wengine? Je, anatumia maneno yasiyo na upendo (unkind) kwa nduguze? Je, anapenda kusema maneno ya kuchokoza wenzake? Je, anapenda kukosoa watu na kuwakejeli (sarcastic)?

Je, anapenda kulitaja jina la Mungu bure? Je, anaonyesha heshima kwako na baba yake kwa maneno yake? Je, maneno yake yanajenga wengine au yanawararua? Je ,anasema lolote limjialo kichwani au anachuja maneno? Je, anamsahihisha aliyekosea kwa unyenyekevu? Je, anatoa ushauri mwema kwa wengine? kufungua kinywa kwa hekima kwa mama au mke ni muhimu. Watoto wanabidi wafundishwe (training) kutii. Hapaswi kuwa mvivu kwa kazi . Twapaswa kufundisha binti zetu jinsi ya kuwa na urembo wa ndani zaidi ya wa nje.